Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Tisa - Tarehe 23 Aprili, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:**

Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Taasisi ya Mifupa Muhimbili kwa Miaka ya 2001, 2002 na 2003 *(The Report of Audited Accounts of the Muhimbili Orthopaedic Institute (MOI) for the years 2001, 2002, 2003)*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 116

**Usambazaji wa Chakula Nchini**

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na upungufu mkubwa wa chakula nchini kutokana na ukame wa mwaka 2002/2003 na kwa kuwa Serikali imekuwa ikipunguza makali ya baa hilo la njaa kwa kutoa msaada wa chakula cha bei nafuu kwa waathirika nchini kote:-

(a) Je, ni kiasi gani cha chakula kimesambazwa kwa waathirika na kiasi gani hakikuwafikia walengwa na ni kwa sababu gani?

(b) Je, Serikali imejifunza nini na ina mikakati gani ya usambazaji wa chakula cha njaa kwa walengwa kwa wakati muafaka endapo likitokea baa lingine la njaa kama hilo?

(c) Je, kuna waathirika wangapi na kutoka wapi waliopoteza maisha yao kutokana na baa hilo la njaa nchini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2004 kiasi cha tani 59,454 za mahindi zilikuwa zimesambazwa nchini katika Wilaya 67 ambazo zipo ndani ya Mikoa 17 zilizohitaji msaada wa chakula. Kati ya tani hizo, kiasi cha tani 32,000 zilitengwa na Serikali na kuuzwa kwa wananchi waliokabiliwa na upungufu wa chakula kwa bei nafuu ya shilingi 50/= kwa kilo.

Aidha, Serikali iliomba msaada wa chakula kwa wahisani na jumla ya tani 27,454 zilitolewa na wahisani kupitia *WFP*. Chakula hicho kiligawiwa bure na mashirika yasiyo ya Kiserikali kwa walengwa. Chakula chote kimewafikia walengwa na kwa wakati muafaka. Aidha, Wizara ya Kilimo na Chakula ilihakikisha maeneo yenye upungufu wa chakula na bei ni ya juu sana yanapelekewa mahindi ya kuuza kwa njia ya biashara ili kupunguza makali ya bei. Jumla ya tani 29,000 zilisambazwa kwa njia hii kwa kuwauzia wafanyabiashara mbalimbali toka *SGR*.

(b) Napenda kusema kuwa, Serikali imejifunza mengi kutokana na baa la njaa lililotukumba mwaka huu. Kubwa ni kwamba wananchi wengi hawajiwekei chakula cha kuwatosha na familia zao kwa muda wote, ndiyo maana hivi sasa Serikali inaendesha kampeni kabambe ya kuhimiza hifadhi ya chakula kwa kila kaya. Serikali kwa upande wake itaimarisha uwezo wa *SGR* ili iwe na akiba ya kutosha kuweza kukabili upungufu wowote wa chakula utakaojitokeza. Aidha, Sera ya Menejimenti ya Maafa ambayo imepitishwa na Serikali wiki hii itaainisha utaratibu mzuri zaidi wa ushirikishaji wadau mbalimbali katika kukabiliana na maafa mbalimbali yakiwemo ya njaa.

(c) Mwisho, napenda kusema kuwa, hakuna mwananchi aliyepoteza maisha kutokana na baa la njaa kwani Serikali kupitia *WFP* imetoa tani 27,454 bure kabisa Vijijini kwa walengwa na tani 32,000 zilizotolewa na Serikali, walengwa walitakiwa kutoa shilingi 50/= tu kwa kilo badala ya gharama halisi ambayo ni zaidi ya shilingi 150/= kwa kilo. Baadhi ya walengwa walioshindwa kutoa kiasi hicho cha shilingi 50/= kwa kilo waliruhusiwa kupewa chakula hicho bila kulipia.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri. Pamoja na majibu haya mazuri, je, Serikali ipo tayari kupokea shukrani za wananchi wa Jimbo langu kwa kupata mahindi ya chakula cha njaa kwa wakati muafaka?

Pili, je, Serikali imeweza kuwapata wakorofi wote ambao wamejaribu kukorofisha au kuleta matatizo katika juhudi hizi ambazo zinafanywa na Serikali za kuokoa wananchi wake? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali napenda kupokea hizo shukrani. Lakini nataka niseme kwamba ingawa amesema wakorofi, lakini mimi nataka nilibadilishe kidogo, niwapongeze sana viongozi wote wa Serikali katika mtandao wa Serikali kutoka Vijiji mpaka Mikoa kwa kazi kubwa waliyofanya ya kushirikiana na wananchi katika kuhakikisha kwamba tatizo hili la upungufu wa chakula linasimamiwa vizuri katika nchi hii.

Nawapongeza vile vile wahisani mbalimbali ambao wametusaidia katika kuongeza uwezo wa chakula katika nchi hii. Ukorofi haukuwepo ambao naweza kuusema hapa, kila aliyetakiwa kuwajibika aliwajibika kwa kadri ya uwezo wake. *(Makofi)*

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa kwenye Mkoa wa Lindi mvua nyingi sana zimenyesha na kusababisha mazao kuharibika na hivi ninavyozungumza bado mvua zinaendelea kunyesha kuashiria kwamba baa la njaa bado litakuwepo na kwamba njaa ya sasa kwa kweli imekwenda likizo. Serikali inalijua hilo na inajiandaa vipi kupambana na balaa jipya la njaa kwa Mkoa wa Lindi ambao mazao yake yameathirika na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba mvua zinaendelea kunyesha katika sehemu mbalimbali na tunafahamu pia baadhi ya sehemu nyingine hazitapata mvua za kutosha kama tulivyotarajia, lakini kwa ufupi ni kwamba Serikali inajiandaa kutuma Tume ya Tathmini nyingine ya Kiserikali mwezi Juni ili kufanya tathmini kama tuliyoifanya mwaka 2003 kuhakikisha kufanya tathmini ya chakula kwa mavuno ambayo yamepatikana kwa msimu huu na matarajio ya upungufu ambayo yanaweza kuonekana katika kipindi hicho. *(Makofi)*

Na. 117

**Kituo cha Afya Kisangara**

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati Waziri wa Afya alipotembelea Kituo cha Afya cha Kisangara katika Wilaya ya Mwanga mwaka 1998 aliahidi kuwa Serikali itakipatia kituo hicho gari la wagonjwa na kwa kuwa utekelezaji wa ahadi hiyo umechukua muda mrefu sasa.

Je, Serikali itakubali kulitatua tatizo hilo katika Bajeti yake ya mwaka 2004/2005?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mbunge wa Mwanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mwaka 1998, Waziri wa Afya aliahidi kutoa gari kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Kisangara, lakini kutokana na ufinyu wa Bajeti hadi sasa gari hilo halijapatikana. Kutokana na umuhimu wa gari hilo, tumeishauri Halmashauri yake ya Wilaya na wameweka makadirio ya kununua gari hilo katika maombi maalum siyo katika maombi ya kawaida kwenye Bajeti ya 2004/2005. Tunayo matumaini makubwa kwamba kama tutashirikiana kusukuma hayo maombi tunaweza kufanikisha ombi la Mheshimiwa Maghembe.

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa magari haya ya *ambulance* ni muhimu sana katika kuokoa maisha ya watu Vijijini hususan katika Vituo vya Afya; na kwa kuwa Vituo vingi vya Afya hapa nchini havina magari hayo ya *ambulance.*

Je, Serikali ina mpango wowote wa kuweka mkakati wa makusudi wa kuhakikisha kwamba magari hayo yanapelekwa katika Vituo vingi vya Afya Vijijini ili kuokoa maisha ya watu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, juhudi za Serikali kutatua tatizo hilo zipo na kwenye Bajeti ya mwaka 2003/2004 tuli-*attempt* kuomba Serikali isaidie ku-*provide* magari kwa ajili ya vituo vyote. Lakini kutokana na ufinyu wa Bajeti mwaka 2003/2004 imeshindikana, lakini bado tunaendeleza mawasiliano tena kwa Bajeti hii tuone kama tunaweza kufanikisha kwa angalau kwa awamu ili tuweze kupunguza tatizo hili. *(Makofi)*

Na. 118

**Waganga na Gari la Wagonjwa Kituo cha Afya cha Iselamagazi**

**MHE. ROBERT J. BUZUKA** aliuliza:-

Kwa kuwa Kituo cha Afya cha Iselamagazi kinakabiliwa na upungufu mkubwa wa Waganga *(RMA, MO)* na Wakunga, pia hakina gari kwa ajili ya kuwahudumia wagonjwa hasa pale inapolazimu mgonjwa kupelekwa Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga:-

(a) Je, ni lini Serikali itapeleka watumishi wenye sifa zinazostahili ili wananchi waweze kupatiwa huduma muhimu na bora?

(b) Je, ni lini Serikali itatoa gari litakalosaidia kubeba wagonjwa na kuwapeleka Hospitali ya Mkoa kwa matibabu zaidi kwa kuwa matatizo ya wagonjwa yanatokea mara kwa mara?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Robert Jacob Buzuka, Mbunge wa Solwa, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Hamashauri ya Wilaya ya Shinyanga ni mojawapo kati ya Halmashauri zilizo katika mpango wa maboresho ya Serikali za Mitaa unaolenga katika kuboresha utoaji wa huduma mbalimbali kwa wananchi.

Chini ya mpango huu uchambuzi wa watumishi wote *(staff audit)* kwa sekta zote ulikwishafanyika. Kwa mujibu wa Ikama na Muundo mpya wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Kituo cha Afya cha Iselamagazi kinapaswa kuwa na jumla ya watumishi 29 lakini waliopo ni 23 na kati ya hao 23, watumishi saba hawahitajiki kituoni hapo na hivyo kufanya watumishi wanaohitajika waliopo kuwa 16 na kuacha upungufu wa watumishi 13 akiwemo *Assistant Medical Officer* mmoja, *Clinical Officer* mmoja, *Nurse Midwife* watatu, *Public Health Nurse* Daraja B watatu, *Pharmaceutical Assistant* mmoja, *Accounts Assistant* mmoja, Dreva mmoja, Dobi mmoja na Mlinzi mmoja.

Aidha, Halmashauri inaendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa ajili ya kupata kibali cha kujaza nafasi zilizowazi katika kituo hicho na pia kuwapeleka katika maeneo mengine watumishi ambao hawahitajiki kulingana na Ikama mpya.

(b) Mheshimiwa Spika, tatizo la vyombo vya usafiri kwa ajili ya Vituo vya Afya linavikabili Vituo vyote vya Afya nchini kikiwemo kituo cha Afya cha Iselamagazi kilichopata gari mwaka 1994. Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta kila namna ya kuweza kutatua tatizo hili sugu angalau kwa awamu. Kwa msingi huo naomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi kufanya subira wakati Serikali inajaribu kutafuta mbinu za kumaliza tatizo hilo.

**MHE. ROBERT J. BUZUKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa Kituo cha Afya cha Iselamagazi kinahudumia eneo kubwa ambapo uhusisha Vijiji vya jirani Wilaya ya Kwimba na hivyo kupelekea upungufu mkubwa wa madawa na vifaa. Je, Serikali kupitia utaratibu uliopo inakubali kuongeza mgao wa madawa na vifaa ili kukidhi mahitaji?

Pili, kwa kuwa utaratibu wa mgao wa fedha za *Basket Fund* hupelekwa katika hospitali za Wilaya kwa uratibu na matumizi. Je, si kweli kwamba Wilaya zisizo na

hospitali za Wilaya hazipati huduma hiyo na kama ni kweli Serikali inafanyaje kwa Wilaya ambazo hazina hospitali zenye hadhi ya Wilaya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza upo utaratibu ambao unatumika katika kuhakikisha kwamba wananchi wa maeneo fulani wanapata madawa angalau yanayowiana na idadi ya watu. Kwa hiyo, taarifa zile za kila mwezi ambazo zinapelekwa katika sekta ya afya au Wizara ya Afya ndiyo hasa za msingi katika kuwezesha kupata madawa yote yanayohitajika. Kwa hiyo, pengine tutahimiza tu taarifa hizo ziweze kukamilishwa kwa haraka ili tuweze kuona namna gani marekebisho yanaweza kufanyika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili ninaloweza kusema tu ni kwamba Mfuko huu wa *Basket Fund* unatumika katika maeneo yote tu wala hauna ubaguzi wa namna yoyote, ndiyo maana Vituo vya Afya na Zahanati pote nchini sasa hizi zipo juhudi za kuzikarabati kutokana na fedha hizo.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, nafurahi kupata nafasi kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Waziri lakini naona lipo tatizo kidogo. Kwa kuwa wananchi wengi wameitika wito wa Serikali kujenga majengo ya zahanati kwa nguvu zao ili wapate huduma za afya na sasa hivi lipo tatizo la kupatikana kwa waganga na zahanati nyingi sasa hivi zimejengwa kama vile zahanati ya Kwekanga kule Lushoto, lakini imeshindikana kufunguliwa kwa kukosa Madaktari. Je, Serikali inatamka nini na itatatua lini tatizo hili? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza tunaomba tu tuwapongeze wananchi kwa ujumla ni kweli kabisa wanafanya kazi kubwa sana ya kujitolea kujenga zahanati, vituo vya afya na hata hospitali katika maeneo mengine. Kwa hiyo, ni juhudi nzuri na Serikali inazitambua. Kuhusu uhaba wa Madaktari au wataalam, kwa ujumla tunajitahidi kukabiliana na tatizo hili si kwamba hawapo, tunao wataalam katika ngazi fulani fulani wa kutosha lakini tatizo ni fedha kwa ajili ya ile *wage bill* inayokuja kujitokeza katika kujaribu kukidhi haja hiyo. Sasa kwa sababu ni suala la kisera, mimi nina hakika litapatiwa ufumbuzi ndani ya vipindi tunavyotarajia.

Na. 119

**Utaratibu wa Uwekezaji wa Miundombinu kwa *BOT***

**MHE. BERNARD K. MEMBE (k.n.y. MHE. PHILLIP A. MAGANI)** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa muda mrefu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa inazungumzia mtindo wa uwekezaji, hususan katika sekta ya miundombinu kwa utaratibu wa *Build, Operate and Transfer* ili kurahisisha maendeleo:-

Je, Serikali inaweza kuwavutia wawekezaji wowote chini ya utaratibu huo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Phillip Magani, Mbunge wa Ruangwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa *Build, Operate and Transfer (BOT)* ni mbinu ambayo Serikali imeamua kutumia kwa kutoa vivutio maalum *(concession system)* ili kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza katika miundombinu ili kuipa Serikali unafuu katika gharama za uwekezaji. Chini ya utaratibu huu, wawekezaji binafsi huruhusiwa kujenga, kuendesha na hatimaye kukabidhi kwa Serikali miundombinu waliyojenga baada ya muda wa makubaliano kumalizika kwa kuingia Mikataba na Serikali.

Mheshimiwa Spika, mkataba wa namna hii humruhusu mwekezaji binafsi kutoza ushuru kwa watumiaji wote wa miundombinu aliyojenga kwa kuzingatia makubaliano ambayo yako kwenye Mkataba na Serikali. Ni kwa njia ya kutoza ushuru ambapo inatarajiwa kwamba mwekezaji ataweza kurejesha gharama na pia kutengeneza faida katika muda wa Mkataba. Ujenzi wa barabara na madaraja ni baadhi tu ya miradi inayoweza kufanywa chini ya utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, chini ya utaratibu huu Serikali imeshaanza majadiliano ya awali na mwekezaji aliyejitokeza ikiwa ni Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* juu ya ujenzi wa Mradi wa Daraja la Kigamboni *(Crossing Proposed Project)* katika eneo lililoko mwisho wa mkondo wa bahari ili kuunganisha Dar es Salaam Kaskazini na Kusini.

Mheshimiwa Spika, miaka ya karibuni imejitokeza Kampuni ya wageni na wazawa ya *PRODECO* ambayo imefanya mazungumzo ya awali na Wizara ya Ujenzi kwa lengo la kujenga barabara kuunganisha Mji wa Dodoma na Nzega kupitia Tabora kilometa 487 na matarajio ya kuunganisha Tabora na Kigoma kilometa 690. Pia barabara nyingine iliyopendekezwa kujengwa kwa utaratibu huu ni ile inayounganisha Mji wa Bagamoyo na eneo la utalii la Saadan kilometa 40 na upo uwezekano wa kuendelezwa hadi Tanga Mjini kupitia Pangani. Miradi mingine iliyofikiriwa ni pamoja na ile ya *Mtwara Development Corridor.*

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa utaratibu huu wa uwekezaji katika miundombinu kwa njia ya *Build, Operate and Transfer* utaweza kuwavutia wawekezaji wengi ili kuboresha sekta ya usafiri nchini.

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, bado ningependa niulize.

Kwa kuwa mpango huu wa *Build, Operate and Transfer* yaani kujenga, kuendesha na kukabidhi ni wa muda mrefu na watu wa *Mtwara Corridor* tuliahidiwa kweli kwamba mpango huu ndiyo ungewezesha kujenga na kuimarisha *Mtwara Corridor.* Je, kuna mradi wowote katika nchi hii ambao unaendeshwa chini ya hii programu ya *BOT* na kama haupo kuna tatizo gani hasa linalofanya Serikali iwe na kigugumizi ku-*adopt BOT?*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali ilipanga baadhi ya miradi itakayojengwa katika Mradi wa *Mtwara Corridor* ijengwe kwa utaratibu wa *BOT* lakini kama tunavyofahamu mradi huu ni mkubwa na una maandalizi mbalimbali ambayo yote yanalenga katika uwekezaji wa miundombinu. Lakini kama nilivyosema awali ni kwamba taratibu hizo Serikali sasa inataka kuzitumia ili kuipunguzia Serikali gharama kwa kujenga miradi mikubwa hasa ile ya miundombinu katika maeneo mbalimbali pamoja na *Mtwara Corridor.*

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo tayari yameshawekewa mipango ya kufanyiwa utaratibu huo ni kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi kwamba kuna daraja la Kigamboni na barabara nilizozitaja. Mpaka sasa hatujaanza na hii kwetu ni dhana mpya ambayo lazima tuifanyie kazi kwa makini zaidi ili tuweze kuitekeleza kwa ufanisi. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima kabisa ningependa kwa niaba ya Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, ningependa kuongeza jibu zuri kabisa alilotoa Mheshimiwa Waziri, lakini kuna kipengele kimoja Mheshimiwa Bernard Membe alikiuliza na nafikiri ni muhimu tukakijibu kwa ufasaha kwamba kuna tatizo gani hasa miradi hii haiendi?

Miradi hii inakwenda kwa *interest* ya nchi, haiwezi kwenda kwa *interest* ya watu binafsi. Tulipata kampuni moja, *Central Corridor Company,* ambayo ilitaka kutengeneza barabara kutoka Itigi kuja Manyoni, wao masharti makubwa waliyoyataka kwa kutengeneza kipande hicho tu, waruhusiwe kuzuia barabara tangu Dar es Salaam mpaka Mwanza ili wao watoze kodi hizo kufidia kujenga kipande hicho.

Pili, walitaka wapewe *road reserve* ya kila upande, huku maili tatu na huku maili tatu, maana yake ingebidi kubomoa hata reli iliyokuwepo hapo. Hayo ni baadhi tu ya masharti ambayo tumeyakataa. Tukasema hayo si *interest* ya Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maria Watondoha, dakika tano za swali hilo zimekwisha, kwa hiyo, tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 120

**Ubinafsishaji Nchini**

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI** aliuliza:-

Kwa kuwa zoezi la ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma limekuwa likiendelea nchini kwa kasi ndogo:-

(a) Je, ni kitu gani kinachosababisha zoezi hilo lisiende kwa haraka kama ilivyokusudiwa?

(b) Je, ni kwa nini mpaka sasa wananchi wa Jimbo la Siha hususan Kata ya *West Kilimanjaro* hawajagawiwa maeneo ya kujenga makazi ya kudumu kama Serikali ilivyoahidi wakiachwa wale walio chini ya *TBL?*

(c) Je, kwa nini Serikali isitoe ratiba maalum kwa wadau wote ili zoezi hilo lianze na kukamilika?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Zoezi la ubinafsishaji linatekelezwa kwa kuzingatia kikamilifu sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa. Aidha, katika kumpata mwekezaji anayefaa inatakiwa taratibu za zabuni zitumike na wadau mbalimbali kuhusishwa katika kutathmini na hatimaye kumpata mwekezaji anayekusudiwa. Kazi hii huchukua muda mrefu kwa vile inatakiwa ifanywe kitaalam na kwa umakini mkubwa sana hasa ikizingatiwa kwamba lengo la ubinafsishaji ni kupata wawekezaji mahiri ambao watashiriki ipasavyo katika juhudi za kujenga uchumi imara wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, inabidi pia ikumbukwe kwamba nchi nyingi za Afrika na kwingineko zinabinafsisha mashirika. Hii ina maana kwamba kuna ushindani mkubwa wa kupata wawekezaji wanaofaa. Sababu nyingine inayofanya ubinafsishaji usiende kwa haraka inatokana na ukweli kwamba mashirika mengi bado yapo katika hali mbaya kifedha na vitendea kazi na yana matatizo mengi na hivyo kushindwa kuvutia wawekezaji kirahisi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na matatizo hayo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Aggrey Mwanri na Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imedhamiria kukamilisha zoezi la ubinafsishaji kwa muda uliowekwa.

(b) Mheshimiwa Spika, suala la wananchi wa Jimbo la Siha hasa Kata ya *West Kilimajaro* kugawiwa maeneo ya kujenga makazi ya kudumu limekwishashughulikiwa

kikamilifu katika ngazi ya Wilaya ya Hai na ngazi ya Mkoa wa Kilimanajaro na pia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Utafiti wa kina ulikwishafanywa kuhusu idadi ya wananchi wanaohitajika kuhamishwa kutoka katika maeneo ya uvamizi katika mashamba ya ngano na wale walioko katika maeneo ya mabondeni. Pia takwimu za wananchi wote ambao wamo katika msitu wa asili wa Engushai na ambao watahitajika kuhamishwa zimekwishapatikana.

Kutokana na kufahamika kwa idadi hiyo ya wananchi wanaohitaji viwanja, shamba lote la Rosylin limepangwa kupimwa viwanja vya makazi na huduma zote za kijamii kama shule, hospitali, viwanja vya michezo na kadhalika. Kwa makazi peke yake vimetayarishwa viwanja vipatavyo 1,090 vya ujazo mbalimbali.

(c) Mheshimiwa Spika, taratibu za kupima viwanja hivyo zinaendelea na kazi hiyo inatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi sita ijayo kuanzia sasa. Hivyo, utaratibu wa ugawaji wa viwanja kwa walengwa utaanza mara moja. Kazi hii itasimamiwa na uongozi wa Wilaya ya Hai akiwemo Mheshimiwa Mbunge mwenyewe kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Serikali.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Naomba pia nimshukuru Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kwa muda mrefu wananchi wa Jimbo la Siha hususan eneo la *West Kilimanjaro* wamekuwa wanasubiri haya yaliyoelezwa na Mheshimiwa Waziri na kwa kuwa inaonekana kwamba kuna haja pia ya kutoa elimu kuhusu suala hili la ubinafsishaji.

Je, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, rafiki yangu atakuwa tayari kuondoka hapa twende wote katika Jimbo la Siha ili akatoe elimu hii na atakuwa tayari pia kupokea barua hii ambayo nimemwandikia kama mwaliko kwa ajili ya kuja katika Jimbo langu ili haya yote aliyoyasema yaweze kutekelezwa kwa muda huo aliouzungumza? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeza sana Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha, kwa kufuatilia suala hili bila kuchoka hatimaye sasa tunafikia hatima yake.

Kama nilivyosema kuanzia sasa na muda mfupi ujao taratibu ambazo nimezielezea katika swali langu la msingi zitafanywa na Serikali. Pili, nakubali kuja Siha kutoa elimu kwa wananchi kuhusu sera nzuri ya CCM ya ubinafsishaji. *(Makofi)*

Na. 121

**Vifo vya Akinamama Wajawazito**

**MHE. JOB Y. NDUGAI** aliuliza:-

Kwa kuwa Bara la Afrika linaongoza duniani kwa vifo vya akinamama wajawazito wanapojifungua (vifo 1,000 kwa kila akinamama 10,000 wanaojifungua); na kwa kuwa tatizo hilo badala ya kupungua limekuwa likiongezeka hapa nchini kwa akinamama wengi kufa wakati wa kubeba mimba, kujifungua na wiki sita baada ya kujifungua:-

(a) Kwa kuwa vile vifo vya uzazi vinaweza kuzuilika, je, ni kwa nini vifo hivyo vinaendelea?

(b) Je, ni Wilaya gani kumi zinaongoza nchini kwa vifo vya aina hiyo na ni kiasi gani kati ya mwaka 2000 hadi 2003?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna vifo vya akinamama wajawazito hapa nchini bado viko juu na vingi vingeweza kuzuilika kama hatua sahihi za dharura zingechukuliwa mapema wakati tatizo linapotokea.

Mheshimiwa Spika, kuna sababu kadhaa zinazosababisha vifo vya akinamama wajawazito wakati wa kujifungua. Sababu hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuchelewa kufanya maamuzi katika familia na jamii katika kusaidia mama mjamzito apatapo tatizo kutokana na haya yafuatayo:-

Kwanza, wengi wa wanawake, pamoja na wanafamilia kutofahamu kwa usahihi vidokezo vya hatari ambavyo vinahitaji huduma ya haraka na hivyo huchelewa kufanya maamuzi ya kumpatia msaada.

Pili, kutokuwa na mipango ya familia na jamii ya kukabiliana na dharura, mfano kujiandaa kujitolea damu, usafiri na kadhalika.

Tatu, kwenda kwa watu ambao hawataweza kumsaidia kwa tatizo alilonalo mfano kifafa cha mimba kwenda kwa mganga wa kienyeji.

(ii) Kuchelewa kupata huduma ya rufaa kutokana na yafuatayo:-

Kwanza, Vituo vya kutolea huduma za dharura kuwa mbali na wananchi.

Pili, uhaba wa usafiri wa uhakika, hasa vijijini, ambapo njia ni mbovu, hakuna magari na sehemu nyingine hasa wakati wa mvua hakuna usafiri wala magari.

Tatu, baadhi ya wananchi kutokuwa na uwezo wa kulipia usafiri kutokana na uwezo.

(iii) Kuchelewa kupata huduma katika vituo vya kutolea huduma kutokana na yafuatayo:-

Kwanza, ukosefu wa upatikanaji wa damu katika hospitali ambao unachangiwa na tatizo la Ukimwi na pili, wanawake kufika katika vituo wakiwa na hali mbaya kwa kuchelewa hivyo inakuwa vigumu kuokoa maisha yao.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na wanawake wengi kujifungulia majumbani, takwimu tulizonazo kutoka vituo vya huduma haziwakilishi vizuri hali halisi ya vifo vilivyotokea katika Wilaya zetu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya kumi zinazoongoza kwa vifo vya akinamama wajawazito ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ngorongoro vifo 1,565 kati ya 100,000, Kongwa vifo 1,448 kati ya 100,000, Morogoro Mjini vifo 907 kati ya 100,000, Shinyanga Mjini vifo 874 kati ya 100,000, Dodoma Mjini vifo 858 kati ya 100,000, Tabora Mjini vifo 774 kati ya 100,000, Bukoba Mjini vifo 771 kati ya 100,000, Mtwara Vijijini vifo 696 kati ya 100,000, Mbeya Mjini vifo 589 kati ya 100,000 na Lindi Mjini vifo 581 kati ya 100,000. Wilaya za Mjini zinaonyesha idadi kubwa ya vifo hivi kwa kuwa hupokea rufaa toka vituo vyake vya Vijijini. Takwimu hizi ni zile zilizotoka kwenye vituo vya kutolea huduma tu na hazijumuishi wale waliojifungulia majumbani.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge washirikiane na Serikali katika mambo yafuatavyo:-

Kwanza, kuwaelimisha wananchi kuhusu suala la dharura na kuwa na Kamati katika Vijiji kwa ajili ya kuwasaidia wanawake wajawazito wanapopata dharura.

Pili, kuhamasisha jamii ili akinamama wajifungulie kwenye vituo vya kutolea huduma na tatu, kuendelea kuhamasisha wananchi kujitolea damu.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, nashukuru sana kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kama alivyosema takwimu nyingi za wanaojifungulia nyumbani bado

hazifahamiki kwa kutegemea wakunga wa jadi ambao wamekuwa wakichangia katika sehemu fulani ya vifo vingi vya akinamama huko vijijini, je, Serikali inasema nini kuhusu wakunga hawa wa jadi?

Pili, kwa kuwa Wizara inao mpango wa kuwamotisha watumishi wake unaoitwa *SASE,* lakini mpango huu umekuwa ukiwafaidisha zaidi Maofisa wa Wizarani, wachache wa Mkoani na watano tu Wilayani. Lakini mpango huu hauwamotishi chochote wale *MCH* ambao wako vijijini wanaozalisha akinamama wajawazito usiku wa manane kwa kandili, je, sasa Wizara inasemaje kuhusu mpango huo wa *SASE* kuwafikia watumishi walioko vijijini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la wakunga wa jadi Serikali inatambua mchango unaotolewa na wakunga wa jadi. Tatizo lililopo ni kwamba wakunga hawa wanatakiwa wapatiwe mafunzo ili watoe huduma zao kwa usahihi zaidi.

Pili, ingekuwa vyema kama wakunga hawa wangejumuishwa katika kutoa huduma zao katika Vituo vya Afya badala ya kutolea majumbani. Kwa hiyo, Serikali inaendelea na utaratibu wa kuwapa mafunzo wakunga wa jadi ambao kwa miaka mingi wamekuwa wakisaidia sana kutoa huduma hizi. Kwa hiyo, kwa mafunzo haya tuna uhakika kwamba ubora wa huduma zao utaongezeka ili hatimaye waweze kupunguza vifo ambavyo sasa hivi vinatokea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la *SASE* nataka niseme katika jambo hili kwamba fedha ambazo zinatolewa kwa ajili ya shughuli hii ni kidogo na hii ni awamu ya kwanza. Awamu ya kwanza imekusudia kulenga watu waliokuwa na majukumu ndiyo maana kila Wilaya kuna watu watano. Utaratibu uliopangwa ni kwamba baada ya awamu hii kila fedha hizi zinapoendelea kupatikana, basi wafanyakazi wengi zaidi watahusishwa ili hatimaye wengi wameweza kupata motisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Anne Nyinamtemi Malecela, subiri kwanza, Mheshimiwa Waziri Mkuu, anataka kutoa majibu ya nyongeza. *(Kicheko)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini napenda niongezee majibu ya nyongeza kwa jibu alilotoa kuhusiana na *SASE. SASE* ulikuwa ni mpango wa muda na wa majaribio. Serikali imeona kwamba mpango huo si endelevu. Kwa hiyo, badala yake Serikali inachofanya ni kuimarisha uchumi na kuongeza mishahara kwa watumishi wote badala ya kulenga watumishi fulani fulani. Kwa hiyo, baada ya kipindi hiki kwa wale walioko kwenye *SASE* kwisha, mpango wa *SASE* hautaendelea, na tutakuwa na mpango wa uboreshaji wa maslahi kwa watumishi wote. *(Makofi)*

**MHE. ANNE KILANGO MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa vifo vingi vya akinamama wajawazito vinasababishwa pia na Malaria; na kwa kuwa Malaria ni ugonjwa ambao una kinga na tiba.

Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuwaelimisha wananchi kuhusu kinga ya Malaria kwa kasi ileile inayofanywa kwenye ugonjwa wa Ukimwi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, elimu kwa upande wa ugonjwa wa Malaria inatolewa. Ndiyo maana hivi sasa kuna utaratibu maalum kabisa kwa akinamama wote wajawazito wanapoenda kliniki hupatiwa dawa kuwakinga na Malaria. Dawa hizi hutolewa si kwa matibabu bali ni kwa kinga. Kwa maana hiyo jambo hili linafanywa kwa juhudi zote na Serikali itaendelea kuwahamasisha watoa huduma za afya katika maeneo yote kuendelea kutoa elimu kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa wa Malaria. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa wale wasiojua jina la Nyinamtemi ndiyo jina la Kigogo alilopewa Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, alipoolewa Ugogoni. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 122

**Ujenzi wa Hospiali ya Rufaa Kanda ya Kusini**

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA** aliuliza:-

Kwa kuwa fedha za msamaha wa madeni zinahimizwa zielekezwe kwenye utoaji wa huduma za jamii kama vile afya, maji, elimu na kadhalika:-

Je, kwa nini fedha hizo zisitolewe kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Rufaa katika Mkoa wa Mtwara ambako eneo limetengwa ili kuwapunguzia wananchi adha ya kufuata huduma hiyo Jijini Dar es Salaam , Mbeya na Moshi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa fedha za msamaha wa madeni zinahimizwa zielekezwe kwenye utoaji wa huduma za afya na huduma nyingine za jamii.

Katika Sekta ya Afya, fedha hizi hutumika na kuelekezwa kwenye kuboresha huduma zilizopo kama kuongeza uwezo wa upatikanaji wa dawa, vifaa vya uchunguzi na uimarishaji wa mawasiliano. Hivyo, fedha hizi haziwezi kutumika katika kujenga hospitali ya Rufaa.

Mheshimiwa Spika, Serikali bado inayo dhamira ya kujenga hospitali ya Rufaa Mkoani Mtwara kwa ajili ya Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma. Hata hivyo, uhaba wa fedha ndiyo kikwazo katika kuitekeleza azma hii.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu kwa sasa inawasiliana na nchi kadhaa wahisani ili watusaidie kujenga hospitali hiyo Mjini Mtwara. Serikali ya Japan imeonyesha nia ya kutusaidia.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Kanda ya Ziwa hospitali ya Rufaa wanayo ya Bugando, Kanda ya Kaskazini, *KCMC,* Kanda ya Mashariki, Muhimbili. Je, Kanda ya Kusini na Magharibi Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kujenga hospitali hizo ili huduma zisambae sawasawa nchini?

(b) Kwa kuwa kuanzia mwaka 1995 tumeongeza mapato kutoka bilioni 25 kwa mwezi mpaka leo zaidi ya bilioni 100. Je, suala hili la kusema kwamba Serikali haina fedha lina mantiki au fedha gani zinazotakiwa tena, kwa nini tusijengewe hospitali hii Mtwara? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, suala hapa si umuhimu, suala la umuhimu lipo na Serikali inatambua hivyo na ndiyo maana tumekuwa tunafanya kila juhudi kuweza kupata fedha za kuweza kujenga hospitali hizo mbili za Rufaa na si moja, ni Kanda ya Kusini na Kanda ya Kati ndiyo ambazo hazina Hospitali za Rufaa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, isieleweke kwamba hatuoni umuhimu. Suala linalozungumziwa hapa ni uwezo. Aidha, nataka nimpe taarifa tu Mheshimiwa Mbunge kwamba baadhi ya Hospitali hizi za Rufaa siyo mia kwa mia ni za Serikali. Kwa mfano, hospitali ya Bugando na ile ya *KCMC* ni hospitali za Mashirika ya Dini. Kwa hiyo, endapo kuna Mashirika ya Dini yatakuwa tayari kutusaidia katika upande wa Kusini na Kati Serikali itakuwa tayari kushirikiana nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kwa nini Serikali iseme kwamba haina fedha. Nataka nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba kweli mapato ya Serikali yameongezeka. Lakini hiyo haina maana kwamba Serikali sasa inaweza ikatimiza matakwa yake yote kwa fedha zinazopatikana. Bado fedha hizo zitahitajika nyingi zaidi hususan katika ujenzi wa Hospitali ya Rufaa. Mheshimiwa Mbunge lazima afahamu kwamba ujenzi wa Hospitali ya Rufaa unahitaji fedha nyingi mno. Kwa hiyo, bado tutaendelea kuzungumza na wahisani huku Serikali ikiwa itachangia endapo tutapata watu wa kutusaidia. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona na kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kuhusiana na uwezo wa Serikali na pia juhudi za Serikali kwenye ujenzi wa Vituo vya Afya na Hospitali. Hospitali ya Sekou Toure, Mwanza sasa inajengwa na tuko katika hatua ya kuiendeleza kuijenga, lakini uwezo ni mdogo. Sasa Serikali

inasemaje kutuunga mkono katika ujenzi wa hospitali hiyo ikiwa ni pamoja na kutupatia vifaa na wataalam itakapokuwa imekamilika? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nataka nichukue fursa hii kupongeza kwa dhati uongozi wa Mkoa wa Mwanza kwa juhudi wanazozichukua ili kupata fedha za kuboresha hospitali yao ya Mkoa ya Sekou Toure.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya imekuwa mara zote inasaidia katika kutoa Bajeti kwa hospitali zetu hizi za Mikoa. Kuna fedha za *Basket Fund* ambazo zinafika huko na kuna Fedha za Miradi ya Maendeleo ambazo zinatolewa kwa Mikoa hii. Kwa hiyo, tunategemea kwamba fedha hizi zitatumika kama mchango wa Serikali katika kuboresha hayo ambayo wanafanya. Aidha, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kutoa migao ya dawa kwa hospitali zetu kama anavyozungumza na pia wafanyakazi wataendelea kulipwa na Serikali kwa kadri ya uwezo wa upatikanaji wa watumishi hao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, mwenye swali linalofuata ameondoa swali lake kutoka kwenye *Order Paper* ya leo. Kwa hiyo, tunaendelea na swali linalofuata baada ya hapo, Mheshimiwa Parseko Kone.

Na. 123

**Usambazaji wa Umeme Mji wa Bukoba**

*(Swali lililotajwa hapo juu liliondolewa na mwuliza swali)*

Na. 124

**Umeme Makao Makuu ya Wilaya**

**MHE. PARSEKO V. KONE** aliuliza:-

Kwa kuwa ni sera ya Serikali kupeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya zote nchini:-

(a) Je, Makao Makuu ya Wilaya ya Simanjiro (Orkesumet) yatapatiwa umeme lini?

(b) Kwa kuwa umeme unazalishwa katika Bwawa la Nyumba ya Mungu; na kwa kuwa kuna vijiji kando kando mwa Bwawa hilo vijiji vya Ngorika, Magadini, Kiruani na Msitu wa Tembo; je, ni lini Serikali itavipatia vijiji hivyo umeme?

**SPIKA:** Mimi sikusikia neno lililoongezwa.

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Makao Makuu ya Wilaya ya Simanjiro (Orkesment) yatapatiwa umeme lini?

**SPIKA:** Lini? *Okay.* Kabadilisha kidogo maana ya swali, lakini kama Mheshimiwa Naibu Waziri una majibu unaweza kuendelea.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, naomba kabla ya sijajibu swali la Mheshimiwa Parseko Vincent Kone, Mbunge wa Simanjiro, nitoe maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ahadi ya Serikali ya kuyapatia umeme Makao Makuu ya Wilaya zote nchini ifikapo mwaka 2005 imetokana na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2000 ambayo katika Ibara ya 51(iii) imeahidi kutoa kipaumbele katika usambazaji umeme katika Miji Mikuu ya Wilaya iliyobaki.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2000, wakati wa Ilani ya Uchaguzi inatolewa, palikuwa na Wilaya 18 ambazo Makao Makuu yake yalikuwa hayana umeme. Kwa mujibu wa idadi hiyo ya mwaka 2000 iliyozungumzwa katika Ilani, Wilaya tano za Geita, Tandahimba, Sikonge, Igunga na Mbarali tayari zimeshapatiwa umeme na ifikapo mwaka 2005 Wilaya zingine sita za Biharamulo, Ngara, Serengeti, Ukerewe, Urambo na Rufiji zitakuwa zimeshapatiwa umeme kutokana na kazi ya kupeleka umeme inayoendelea hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, aidha, kazi za awali za kufikisha umeme katika Makao Makuu ya Wilaya za Kilindi na Bukombe zimeshaanza, kwa kazi inayofanywa sasa ya kufikisha umeme Kwediboma ukiwa njiani kuelekea Songwe Mjini wa Wilaya ya Kilindi na ujenzi wa *Sub-station* na usambazaji umeme huko Ilogi na Bugarama kama hatua ya awali ya kuelekea Bukombe.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, katika Wilaya 18 za mwaka 2000, Wilaya 13 zitakuwa ama zimeshafikishiwa umeme au zitakaribia kupata umeme ifikapo mwaka 2005, ikiwa ni sawasawa na asilimia 72.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Parseko Vincent Kone, kama nilivyosema awali, Mbunge wa Simanjiro, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kupatia umeme Mji wa Orkesmet ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Simanjiro, itabidi kujenga kwanza kituo cha kupoozea umeme kutoka Msongo wa umeme 66 kuja 33 katika eneo la kituo cha Nyumba ya Mungu. Pili, kujenga laini ya umeme wa kilovolti 33 yenye urefu wa kilometa 105 toka Nyumba ya Mungu hadi Orkesmet na kilometa 46 toka Lendenai hadi Namalulu. Kazi nyingine ni kufunga transfoma katika Mji wa Orkesemt, vijiji vya Lemkuna, Lendenai, Naberera na Namalulu pamoja na kuwaunganishia wateja umeme.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchelewa kutokana na upatikanaji wa fedha ambazo zinakadiriwa kuwa shilingi bilioni 4 zinazohitajika kwa mradi huo, sasa Serikali

ya Sweden kupitia Shirika lake la *SIDA ,* imeonyesha nia dhabiti ya kufadhili mradi huu na kutokana na majadiliano yanayoendelea Simanjiro inatarajiwa kupata umeme kati ya 2005 na 2006. Tayari upembuzi yakinifu umekamilika Machi, 2004 na mradi huo wa Simanjiro sasa uko *SIDA* Dar es Salaam kwa ajili ya kupatiwa fedha.

Mheshimiwa Spika, vijiji vya Ngorika, Magadini, Kiruani na Msitu wa Tembo vitapatiwa umeme wakati wa utekelezaji wa mradi wa kufikisha umeme Orkesment, Wilayani Simanjiro kama ilivyokuwa katika Wilaya zingine tulipokuwa tunafikisha umeme.

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja ndogo la nyongeza.

Kwa kuwa *TANESCO* imepanga kutumia shilingi bilioni 50 mwaka 2004 kwa ajili ya kurekebisha mfumo wa usambazaji umeme Mkoa wa Kilimanjaro na Arusha; na kwa kuwa zinatakiwa shilingi bilioni 34 tu kuweka umeme katika Mkoa wa Kigoma ambazo zitajumlisha Wilaya tatu.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri hawezi kuishauri *TANESCO* ikaelekeza hizo shilingi bilioni 50 ikazipeleka Mkoa wa Kigoma ili Wilaya tatu zipate umeme na kupata asilimia zaidi ya 80 ya ahadi ya CCM na hapo hapo kuweza kupatiwa megawati karibu 40 kuingia kwenye Gridi ya Taifa badala ya kung’ang’ania kule Kilimanjaro? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza mimi sina taarifa za kwamba *TANESCO* ina shilingi bilioni 50 za kuboresha miundombinu ya umeme kwa Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro tu. Ninachofahamu ni kwamba upo mpango wa kuboresha miundombinu ya umeme ili kuondokana na tatizo la kukatikakatika kwa umeme na kama nilivyoeleza hapa Bungeni wiki iliyopita mpango huu una sehemu mbili.

Sehemu ya kwanza, ni kwa ajili ya kuboresha njia kuu za umeme kwa maana ya hii misongo mikubwa ya 220, 132 na 66 na sehemu ya pili ni kwa ajili ya njia ndogo za umeme za msongo wa 33, 11 na kadhalika katika maeneo mbalimbali nchini na ni mpango wa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, nilisema hapa kwamba utaratibu huu wa kuboresha njia hizi katika mipango ya *TANESCO* ni kama *Relief Projects* ni muhimu katika kuhakikisha kwamba upatikanaji wa umeme unakuwa na uhakika. Ni mpango wa nchi nzima hauhusu Mkoa wa Arusha na Kilimanjaro tu na kama nilivyosema awali sina taarifa za hizo shilingi bilioni 50 anazozisema Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa umeme katika Mkoa wa Kigoma tumeueleza mara nyingi. Napenda nimalize kwa kusema kwamba asilimia hii 72 ambayo tumeifikia sasa nadhani ni muhimu kwa upande wetu sisi na hasa Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kujivunia mafanikio ambayo Serikali imeyapata kwa wakati huu.

Sasa ni wakati wa kuonyesha mafanikio yetu na asilimia 72 kwa hakika ni mafanikio mazuri. *(Makofi)*

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa katika swali la msingi linaulizia juu ya Makao Makuu ya Wilaya ambazo hazina umeme. Makao Makuu ya Wilaya ya Mbinga ni Wilaya ya zamani na haina umeme. Je, Serikali inasema ni lini Makao Makuu ya Wilaya ya Mbinga yatapatiwa umeme? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, katika mpango wa kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya. Wilaya ya Mbinga imepangwa kati ya mwaka 2004 na 2005. Napenda niseme kwamba hatua muhimu katika kufikisha umeme wa gridi hasa katika Mkoa wa Ruvuma ni ya ujenzi wa *Sub-station* pale Makambako.

Napenda niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, sasa fedha zimepatikana za ujenzi wa *Sub-station* ya Makambako kama ndiyo hatua muhimu na ya awali kabisa ya kufikisha umeme katika Mkoa wa Ruvuma ikiwemo Wilaya ya Mbinga, bila ujenzi wa *Sub-station* hiyo isingewezekana kabisa. Serikali imefanya jitihada zote kuhakikisha kwamba fedha zinapatikana na kazi inatarajiwa kuanza wakati wowote kuanzia sasa.

Na. 125

**Stahili za Waliopigana Vita ya Pili ya Dunia**

**MHE. BENSON M. MPESYA** aliuliza:-

Kwa kuwa tunao mashujaa wengi waliopigana Vita vya Pili ya Dunia, akiwepo mzee Tungesye Kang'obe wa Iyunga Mbeya; na kwa kuwa wazee hao wanadai fedha iliyotolewa na Serikali ya Uingereza kama ahsante yao:-

(a) Je, ni lini Serikali italipa stahili za wazee hao?

(b) Kwa kuwa umri wa wazee hao umekuwa ni mkubwa mno, je, isingekuwa vyema stahili hizo wakalipwa mapema?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la namba 125 la Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a) na (b), napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Wakati wa utawala wa Kiingereza wananchi kadhaa walichukuliwa na kujiunga na Jeshi la Kiingereza lililopigana Vita Kuu ya Pili ya Dunia kwa miaka ya 1939 hadi 1945. Wananchi hao walirudi nyumbani baada ya kumalizika kwa vita hiyo.

Kwa kuonyesha shukrani kwa wananchi hao, Serikali ya Uingereza ilifanya yafuatayo:-

(i) Ilijenga majumba ya burudani *(Welfare Centres)* katika kila Wilaya kwa ajili hiyo.

(ii) Ilianzisha Chama cha *British Commonwealth Ex-Services League (BCEL)* chenye Makao Makuu Jijini London - Uingereza na matawi yakafunguliwa katika kila nchi iliyotoa askari. Tawi la Tanganyika ambalo sasa linajulikana kama Tanzania linaendelea kuitwa *Tanzania Legion and Clubs* lenye Makao Makuu yake katika makutano ya Mtaa wa Msimbazi na barabara ya Morogoro.

(iii) Ilianzisha utaratibu wa kuwapatia fedha kidogo wapiganaji wake kwa ajili ya kujikimu *(Benevolence Fund)* chini ya Chama cha *BCEL.*

Baada ya Uhuru maslahi na shughuli za askari waliopigana Vita Kuu ya Pili zilikabidhiwa kwa uongozi wa *TLC.* Fedha za kujikimu ziliendelea kutolewa mpaka mwaka 2000 ambapo *Tanzania Legion and Clubs* ilisimamishwa uanachama wa *BCEL* kwa madai ya uongozi mbaya na ubadhirifu wa fedha. Aidha, *BCEL* ilisimamisha utoaji wa fedha za msaada kwa *TLC* kuanzia mwaka 2000 hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mpesya, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Wizara yangu imepokea malalamiko ya wazee waliopigana Vita Kuu ya Pili kutoka sehemu mbalimbali hapa nchini na tayari tumeanza kuyashughulikia matatizo ya uongozi na ubadhirifu wa fedha na mali nyingine ndani ya *Tanzania Legion and Clubs (TLC).* Tunajitahidi pia kuupatanisha uongozi wa *TLC* na wanachama wa tawi la Dar es Salaam ili *BCEL* iweze kurejesha msaada wa fedha za ahsante kwa lengo la kuwanufaisha walengwa wote toka sehemu mbalimbali. Mara baada ya kazi hiyo kukamilika, ni tegemeo la Wizara yangu kuwa wazee wote akiwemo mzee Tungesya Kang'obe wa Mbeya Mjini watanufaika na msaada huo.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa wakati wazee hawa wanafuatilia fedha hizi walikuwa ni zaidi ya 20 pale kwangu. Sasa nasikitika kusema kwamba nusu ya wazee hao wameshakufa. Je, Serikali haioni umuhimu pamoja na juhudi zote inazozifanya za kufuatilia kuhakikisha kwamba wazee hao wanalipwa malipo yao mapema zaidi kabla hawajatutoka duniani?

La pili, Mheshimiwa Waziri katika jibu lake amezungumza kwamba fedha zile zilisimamishwa. Lakini katika mwezi wa Machi, tulipotembelewa na Balozi wa Uingereza alikiri kwamba wao hata siku moja hawajawahi kusimamisha fedha za wazee hawa na bado wanazileta. Je, tuamini lipi sasa hizo fedha zinameenda wapi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, Serikali inasikitika kwamba wazee wetu wale 20 nusu yao karibuni wamekufa, tunatoa pole na Mungu azilaze roho za marehemu hao mahali pema peponi.

Lakini la pili, ni kwamba tufanye haraka ili waliobaki walipwe fedha zao. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Benson Mpesya, kwamba kwa kweli Serikali itajitahidi kuhakikisha kwamba hii hatua iliyobaki kukamilisha kusuluhisha mgogoro huo wa uongozi unakwenda kwa kasi inayotakiwa. Hata leo asubuhi tulikuwa tunaongea na Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, tukimaliza Bunge hapa tukakae sisi Mawaziri tuwaite watendaji wetu ili tuone njia ambayo tunaweza tukapita ya haraka kuhakikisha kwamba mgogoro huo unakwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Balozi wa Uingereza alipotembelea kule alisema kwamba wao hawajasimamisha kuleta fedha hata mara moja. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha zimesimamishwa hawazileti, isipokuwa kuna ndugu yetu mmoja Ali Sykes, yeye alitengeneza utaratibu wa kuwa anapokea baadhi ya fedha na kuwalipa wazee wa Dar es Salaam. Sasa waliopigana vita siyo wazee wa Dar es Salaam peke yao. Tunahitaji kupata fedha zile ambazo bado ziko kule ili ziletwe katika nchi wazee wote walipwe. *(Makofi)*

**MHE. ISSA MOHAMED SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa *Club* ya Askari wazee ya *Tanzania Legion and Clubs* iliyoko Dar es Salaam ilianza mtafaruku toka mwaka 1997 baada ya kuvamiwa na walowezi, wajanja na matapeli ya Jijini Dar es Salaam. Kwa hiyo, mpaka hii leo Askari wazee waliopigana Vita ya Pili ya Dunia wanasimangwa sana na walowezi waliovamia pale. Serikali kila siku inaunda Kamati ya kufuatilia mtafaruku ule mpaka hivi sasa. Je, Serikali imefikia wapi kuhusu maamuzi yaliyotolewa na Kamati hizo zilizokuwa zikifuatilia migogoro ya pale? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nimesema ni kweli mtafaruku upo na sisi kama Serikali tumeanza kuushughulikia kwanza kwa kujua chanzo chake ni kipi. Chanzo chake ni mtafaruku ambao unatokana na ubadhirifu wa fedha kwa baadhi ya viongozi waliokuwepo. Tukaitisha uchaguzi bahati mbaya kama ilivyo katika maeneo mengine ya *NGOs* hizi wale wale viongozi wabadhirifu wakarudi. Kwa kushirikiana na *British Commonwealth Ex-Services League* tukatengeneza mazingira ikabidi wale viongozi wabadhirifu wakatoka.

Baada ya kutoka sasa ndio tukafanya tathmini mpya tukawapeleka wakaguzi wa ndani wameleta hesabu ya kuonyesha ubadhirifu uko wapi na kiasi gani cha fedha, mali

gani zimeharibiwa na hivi sasa tumekabidhi baadhi ya mambo hayo kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani ili hatua za uchunguzi zaidi zifuatiliwe na wanaopaswa kushtakiwa washtakiwe.

Kwa hiyo, ndiyo hatua tumechukua kama Serikali. Lakini baada ya hapo tunakusudia vile vile kuitisha uchaguzi mpya ili kuondoa kabisa migogoro huu. *(Makofi)*

Na. 126

**Zanzibar - Mwanachama wa *CAF***

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa Zanzibar sasa imekuwa mwanachama rasmi wa Shirikisho la Soka la Afrika *(CAF);* na kwa kuwa ligi ya Muungano inaunganisha nchi hizo mbili katika nyanja za kisoka:-

(a) Je, upo utaratibu mwingine wa kuzikutanisha nchi hizo mbili kisoka?

(b) Je, tufanyeje kama Taifa moja la Tanzania katika kujiinua kisoka?

(c) Je, ni uhusiano gani utakaounganisha vyombo viwili vya *ZFA* na *FAT?*

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Nungwi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuzikutanisha timu za soka za Bara na Visiwani umekuwepo hata kabla ya ligi ya Muungano kuanzishwa. Utaratibu huo wa siku nyingi ni pamoja na kuwepo michezo ya kirafiki kwa timu za Bara kucheza Visiwani za zile za Visiwani kucheza Bara.

Mbali ya Michezo ya Kirafiki, timu za pande zote mbili zinaendelea kukutana kwa zamu katika michezo ya Pasaka. Hata hivyo, bado nafasi ipo kwa Vyama vyetu vya *FAT* na *ZFA* kutafakari upya namna ya kuanzisha mashindano mapya yatakayochukua nafasi ya Ligi ya Muungano na kwa mahitaji yaliyopo.

(b) Mheshimiwa Spika, yapo mengi tunayoweza kufanya ili kuinua soka ya Tanzania. Kati ya hayo ni wadau wote wa soka kukaa chini na kubainisha wazi matatizo yaliyopo, kuyakubali na kuweka mikakati ya kutatua matatizo hayo. Tatizo kubwa kwa wadau wengine wa soka wanayoona wao ni yale wanayoyafikiria wao tu, baadhi siyo wakweli na wanajali zaidi maslahi binafsi kuliko maslahi ya wengi.

Endapo tutaondokana na ubinafsi, tukakubali kukosolewa na kukosoa kwa nia ya kujenga, basi tutaweza kupata mipango mizuri inayotekelezeka na kuinua mchezo wa

soka hapa nchini Tanzania. Ni lazima kwanza watu tukubali kubadilika. Serikali kwa upande wake inajizatiti katika kujenga miundo mbinu ya kisasa ya michezo ikiwemo michezo ya mpira wa miguu na pia kuongeza utoaji wa fedha katika michezo.

(c) Mheshimiwa Spika, uhusiano uliokuwepo kati ya *FAT* na *ZFA* bado upo na utaendelea kuwepo. *FAT* na *ZFA* wamekuwa wakiendesha mashindano ya Ligi Kuu ya Muungano kwa maelewano kati yao na hadi sasa hakuna kizuizi chochote cha kuweza kusababisha kuondoa uhusiano kati yao.

Aidha, pamoja na Zanzibar kupata uanachama wa *CAF,* bado yapo mashindano mengine mengi kama vile Kombe la Dunia, Michuano ya Olimpiki, Michezo ya *SADC* ambapo Bara na Visiwani tunawakilishwa na timu moja tu. Aidha, *FAT* na *ZFA* pia wataweza kushirikiana katika kuandaa michezo itakayoandaliwa na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki hapo baadaye. Kwa hiyo, suala la kuendeleza uhusiano kati ya vyama hivi viwili haliepukiki.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii kuuliza masuala mawili madogo ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nauliza, kama alivyosema kuwa uhusiano uliopo hivi sasa kwa kweli ni wa mgogoro na matatizo hasa ushiriki wa Mtibwa na Simba. Je, Serikali inalishughulikiaje katika Wizara hizi mbili baina ya Wizara ya Elimu Zanzibar na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo Bara?

Pili, je, katika mafanikio siku zote katika jamii ya watu kunakuwa na pongezi tafrija au viburudisho vya kuhakikisha kuwa hili jambo limefanyika. Je, *ZFA* imefanya hivyo kwa kupata uanachama wa *CAF? (Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ushiriki wa Simba na Mtibwa, yapo masuala ya kiutendaji ambayo yanasimamiwa na *FAT* na *ZFA.*Walikaa pamoja wakajadiliana kwamba katika mgogoro uliojitokeza wa baadhi ya klabu kwenda Mahakamani na kwamba ni lazima nchi iwasilishwe, wakatafuta utaratibu ambao waliona kwamba ni muafaka, wakaiteua Simba na Mtibwa. Kwa hiyo, ilikuwa ni katika kuzingatia mazingira halisi yaliyokuwa yamejitokeza kwa wakati ule. Vinginevyo nchi yetu isingewasilishwa kabisa.

Kwa hiyo, wakatafuta klabu ambazo zina hadhi za kuwakilisha nchi hii katika Uwanja wa Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lile la pili kwa kweli mimi sijalielewa lile la tafrija. Naomba arudie kama inawezekana. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Hebu rudia swali lako la pili.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nilisema hivi katika jamii yoyote ile mnapopata mafanikio lazima mnakuwa na shughuli au tafrija au pongezi ambazo mnapeana baina ya mafanikio.

Je, *ZFA* au Wizara ya Elimu Zanzibar imefanya hivi kuipongeza Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Bara?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, katika hili waliofanikiwa ni *ZFA,* katika hili waliofanikiwa ni Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, tulioandika pongezi ni sisi Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kumpelekea Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni na Michezo kumpongeza yeye na *ZFA* Zanzibar.

**MBUNGE FULANI:** Sasa chakula?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Chakula hilo bado, lakini pongezi tumeshatuma. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza suala moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kila siku tunavyokwenda katika nchi hii hali ya michezo inazidi kushuka kutokana na ubabe wa Ndolanga. Je, Mheshimiwa Waziri atatuthibitishia hapa kwamba Ndolanga ndiye kiboko wa nchi hii katika mpira wa miguu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza si kweli kwamba hali ya michezo katika nchi hii inaendelea kushuka.

Mheshimiwa Spika, nataka nirudie Waheshimiwa Wabunge katika ngumi Afrika tunaongoza. Katika Kriketi timu ya Wanawake imechukua kombe la Afrika na kupitia Bunge lako Tukufu naomba kuwapongeza sana timu ya Kriketi ya Wanawake kwa kutuletea ushindi.

Katika riadha tulipokwenda Manchester tumerudi na medali za fedha, dhahabu na shaba. Tumekwenda *All Africa Games* tulikuwa na wachezaji 17 lakini tumeshika nafasi ya 16 ukilinganisha na nchi kama Afrika ya Kusini ilipeleka wachezaji 950, Nigeria 600 na katika hao 17 sisi tukaweza kutoa wachezaji wanne...

**SPIKA:** Naomba utulivu Bungeni.

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Katika wachezaji wanne walioteuliwa kuunda timu huko Hortative bado ni wazuri zaidi. Katika wanariadha bora zaidi duniani 50, 11 wanatoka Tanzania. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tatizo tulilonalo ni katika mpira wa miguu. Sasa unapojumuisha kabisa ukasema kwamba hali ya michezo inashuka Tanzania si kweli huifanyii haki nchi yako. Hii ndiyo wanazungumza sana wenzangu Waandishi wa Habari nasema yale tunayofanya vizuri hivi kwa nini hamuipongezi nchi hii kwa nini hamjivunii, kwa nini hatutembei kifua mbele? *(Makofi)*

Sasa nakuja kwenye suala la Ndolanga. Ndolanga si kiboko cha nchi hii. Ndolanga ni raia kama raia mwingine yeyote, anafuata sheria za nchi hii isipokuwa kuna suala linaonyesha demokrasia. Mwanzoni mwa wiki hii hapa wakati Kamati ya Maendeleo ya Jamii ilipokuwa ikijibu hoja kuhusu *FAT* inavyoharibu mchezo wa mpira wa miguu tulieleza au Mwenyekiti wa Kamati ile alieleza wazi wazi kwamba tunaopaswa kuanza kusahihisha hali ile ni kuanzia sisi Waheshimiwa Wabunge tunaotoka katika Wilaya na Mikoa. Wanaokuja kumchagua Ndolanga wanatoka katika Wilaya na Mikoa. Kwa nini hatuendi kuwaambia kwamba jamani wakati umefika wa kubadilisha uongozi. Tunasubiri demokrasia imefanya kazi yake tunakuja hapa tunasema sasa Serikali ina msimamo gani.

Mheshimiwa Spika, nilishasema tangu awali kwamba hata kama Jimbo la Uchaguzi ikaleta Mbunge ambaye ni tatizo Spika hawezi kumfukuza Mbunge yule wala Serikali haiwezi kumfukuza Mbunge yule, itabidi waishi naye na Jimbo lile mpaka mwisho wa miaka mitano. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 127

**Walimu Kutoshiriki Masuala ya Siasa**

**MHE. GRACE S. KIWELU (k.n.y. MHE. PHILLEMON NDESAMBURO)** aliuliza:-

Kwa kuwa walimu ni watu waelewa na wanaominiwa sana na jamii, na upeo wao wa uelewa unatoa mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi na Taifa kwa ujumla; na kwa kuwa upo waraka unaowakataza walimu hao kushiriki katika masuala ya siasa kama viongozi wa mitaa na madiwani:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa waraka huo umepitwa na wakati na kwamba sasa ni muda muafaka wa kuufuta?

(b) Je, kuwanyima wenye upeo wa kushiriki katika maamuzi ya maendeleo ya nchi yao sio kurudisha nyuma maendeleo yao na ya nchi kwa ujumla?

(c) Je, waraka huo hauvunji haki za binadamu na je, hiyo ndiyo demokrasia na utawala bora?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Phillemon

Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, lenye sehemu (a), (b) na ( c) napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa mwaka 2000 unaohusu Maadili ya Watumishi wa Umma wakiwemo walimu katika mfumo wa Vyama vingi vya Siasa walimu wanaruhusiwa kushiriki katika mambo ya siasa kama wakipenda.

Hata hivyo kwa kuwa hakuna haki isiyo kuwa na wajibu wala uhuru usiokuwa na mipaka, walimu kama Watumishi wa Umma wanaruhusiwa kushiriki katika mambo ya siasa kwa utaratibu maalum ili kuhakikisha kwamba wanazingatia maadili ya msingi ya utendaji wa kazi zao. Walimu wanaweza kushiriki katika shughuli zifuatazo:-

- Kuwa mwanachama wa Chama cha Siasa anachokipenda.
- Kupiga kura kwenye Uchaguzi wa Rais, Wabunge na wa Serikali za Mitaa.
- Kuhudhuria Mikutano halali ya kisiasa nje ya saa za kazi.
- Kutoa michango yao binafsi kwa ajili ya chama chake akiwa nje ya mahali pa kazi na nje ya saa za kazi.

Mwalimu yeyote endapo ataamua kugombea nafasi yoyote chini ya Katiba au uongozi wa ngazi yoyote katika Chama cha Siasa kwa mujibu wa waraka huo, Utumishi wa Mwalimu huyo utahesabiwa kuwa umekoma tangu tarehe Tume ya Taifa ya Uchaguzi itakapomtangaza kuwa mgombea uchaguzi au tarehe yake ya kujiandikisha kugombea uongozi katika Chama cha Siasa au siku Tume ya Taifa ya Uchaguzi itakapomtangaza kuwa Mbunge au Diwani. Endapo Mwalimu huyo atashindwa katika uchaguzi na akataka kurejea katika Utumishi hana budi kuomba ajira upya kwa mamlaka zinazohusika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo napenda sasa kujibu sehemu (a), (b) na (c) ya swali kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali bado inaona waraka huu unafaa, kwa sababu haumnyimi mwalimu yeyote haki ya kushiriki katika siasa kama akipenda na ushahidi wa wazi ni idadi kubwa ya walimu walio wajumbe wa Bunge hili hivi sasa.

Kwa kuwa Mwalimu ni mtumishi anayehudumia watu wote bila kujali itikadi yoyote, anaweza kushiriki masuala ya siasa huku akizingatia kuwa hafanyi hivyo wakati wa saa za kazi na akiwa mahali pa kazi na akiwa kazini havai sare za chama chochote cha siasa. Aidha, mwalimu haruhusiwi kuajiriwa katika Chama cha Siasa wakati akiwa bado mwalimu. Utaratibu huu uliowekwa ndiyo unaozingatia demokrasia ya kweli katika Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa na haumnyimi haki mwalimu au kuvunja haki za binadamu kama Mheshimiwa Mbunge alivyokuwa anadhani kabla ya maelezo haya.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniruhusu niulize swali dogo la nyongeza.

Katika majibu ya Mheshimiwa Waziri tunashukuru, lakini katika utaratibu wa kuangalia Madiwani ambao wanagombea wanaambiwa wawe na kazi zinazowafanya wajitegemee na ndiyo maana hawalipwi mshahara. Sasa maana yake nini ukilinganisha na maelezo aliyoyatoa kwamba ukitaka kugombea ujifute, je, Diwani huyu ni lazima awe mkulima au mfanyabiashara asiwe mwalimu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (UTUMISHI):** Mheshimiwa Spika, Utumishi wa Umma unapaswa tu usifungamane na itikadi yoyote ili wananchi wote wa itikadi mbalimbali waendelee kuwa na imani ya Utumishi wa Umma, ni kutokana na msingi huo.

Mheshimiwa Spika, Watumishi wa Umma hawaruhusiwi kuwa wawakilishi wa kuwakilisha vyama vyao katika uongozi. Kutokana na kwamba Madiwani hawapaswi kulipwa, ni kwamba kazi hii ya Utumishi wa Umma na kazi zingine ni kazi vile vile kama kazi ya kilimo, biashara ya viwanda nayo ni kazi. *(Makofi)*

Na. 128

**Wanaume Wanaowapa Mimba Wanafunzi**

**MHE. LYDIA T. BOMA** aliuliza:-

Kwa kuwa watoto wengi wa kike hasa wale ambao wazazi wao ni maskini hapa nchini hawapati elimu ipasavyo kutokana na kupata mimba na hatimaye kulea watoto wao:-

(a) Je, kuanzia mwaka 2000 hadi 2003 ni wanaume wangapi wameshtakiwa kwa kitendo cha kuwapa mimba wanafunzi na kuwakatiza masomo yao?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani za dhati za kukomesha vitendo hivyo ili kumnsuru mtoto wa kike?

(c) Kama wapo wanaume ambao wameshtakiwa, je, ni wangapi na kati ya hao ni wangapi walichukuliwa hatua za faini au kufungwa?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lydia Boma, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2003, jumla ya wanafunzi 41,554 sawa na 0.64% ya wanafunzi wote wa Shule za Msingi walikatisha masomo kwa sababu mbalimbali. Kati yao waliokatisha masomo kwa sababu ya kuwa na mimba walikuwa 2,227 sawa na 5.4% ya wanafunzi 41,554 waliokatisha masomo ni 0.07% tu ya wanafunzi wote wasichana wa mwaka huo.

Wizara yangu haijaweka utaratibu wa kutunza takwimu za wanaume walioshtakiwa, kutozwa faini au kufungwa kwa kosa la kuwapa mimba wanafunzi kwa sababu masuala ya kisheria hayashughulikiwi na Wizara yangu. Hata hivyo kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 iliyotungwa na Bunge hili kifungu 35(4) kinampa uwezo Waziri anayesimamia masuala ya elimu kutunga kanuni inayoainisha makosa na adhabu kwa mtu yeyote anayesababisha mwanafunzi kuacha shule.

Kutokana na uwezo huo hivi karibuni imetungwa kanuni mpya iitwayo *The Education (Imposition of Penalties to Persons who marry or impregnate a school girl) Rules 2003,* inayotoa adhabu ya kifungo kisichopungua miaka 3 na isiyozidi miaka 6 bila faini kwa mwanaume yeyote anayempa mimba mtoto wa shule.

Wizara yangu imetoa maelekezo kwa Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya kwa njia ya Waraka wa Elimu Na. 6 wa mwaka 2004 wa tarehe 15 Aprili, 2004 waanze kuwachukulia hatua wote wanaowapa mimba watoto wa shule na taarifa za hatua hizo zirekodiwe na kuwasilishwa Wizarani.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kumnusuru mtoto wa kike kutokana na kukatisha masomo kwa sababu za mimba, Serikali inachukua hatua zifuatazo:-

(i) Kama nilivyosema katika sehemu (a) ya jibu, Serikali imetunga kanuni mpya inayotoa adhabu ya kifungo cha miaka 3 lakini isizidi miaka 6 bila faini. Narudia bila faini kwa mwanaume yeyote anayempa mimba mtoto wa shule na ni matumaini yangu kuwa Mahakimu hawatasita kuwatupa Gerezani kwa miaka 3 au 6 yeyote anayefanya kosa hilo.

(ii) Wizara inasisitiza utoaji wa huduma za malezi na ushauri nasaha katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu. Afisa Elimu Kiongozi ametoa Waraka wa Elimu Na. 11 wa Mei, 2002 unaohusu uanzishaji wa huduma za malezi na ushauri nasaha Mashuleni na Vyuoni.

(iii) Elimu ya Familia pamoja na Elimu dhidi ya Ukimwi inatolewa kwa walimu ili waweze kuwapa wanafunzi stadi za maisha za kuweza kuepuka mienendo na mazingira hatari yanayoweza kusababisha wapate mimba pamoja na maambukizi ya magonjwa ya ngono.

(c) Mheshimiwa Spika, jibu la sehemu (c) ya swali ni kama nilivyosema katika sehemu (a) hapo juu. *(Makofi)*

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa watoto wa shule wanaume pia wanawapa mimba wanafunzi wa kike na kukatishwa masomo, je mwanafunzi wa kiume akibainika amempa mimba mwanafunzi wa kike anachukuliwa hatua gani?

Kwa kuwa Waziri alipokuwa anajibu swali la msingi anasema kwamba hawezi kufuatilia kwa wakati huo jinsi gani wanafunzi wanaume wameweza kushtakiwa na waliowapa mimba.

Je, atajuaje haki kama inatendeka kwa wanawake. Tathmini ya Serikali itaweza kupatikanaje kuona haki za wanawake zinatendeka sawa na Serikali inavyohitaji elimu kwa wote? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu watoto wavulana waliowapa mimba wasichana, hawa nao wanafukuzwa shule kwa sababu kumpa mimba msichana kabla hujamwoa hata kama sio mtoto wa shule sio maadili mema. Shuleni tunafundisha vijana wetu kufuata maadili mema.

Katika makosa yale ya kufukuzwa shule ni pamoja na kosa la kutokuzingatia maadili mema katika jamii. Kwa hiyo, mvulana aliyempa mimba msichana wa shule naye hatua ya kinidhamu naye anafukuzwa shule. Kwa hiyo, hakuna ubaguzi wowote katika suala hili la mimba.

Sasa swali la pili kwamba nimesema siwezi kufuatilia. Nadhani majibu yangu hayakuandaliwa vizuri tu kwa sababu kama Mheshimiwa Mbunge amenisikiliza vizuri.

Nimesema sasa tumetunga kanuni mpya hii niliyoitangaza hapa na katika kanuni ile tumewapa wajibu Wakuu wa Shule na Maafisa Elimu kutuletea *data.* Wao ndio wanaochukua hatua za kuanzisha kesi Mahakamani na kuanzia hii *circular* na kanuni hii ya mwaka huu wanahitajika kuleta Wizarani *data.* Kwa hiyo, kuanzia mwaka huu nitakuwa na uwezo wa kutoa *data* zinazohitajika katika suala hili katika Bunge hili.

Na. 129

**Uuzaji wa Zao la Korosho**

**MHE. OMAR S. CHUBI** aliuliza:-

(a) Je, kati ya mwaka 2001 hadi 2003 Mikoa ya Mtwara na Lindi imeuza tani ngapi za Korosho na kiasi gani cha fedha kimepatikana kuchangia Pato letu la Taifa?

(b) Je, wakazi wa Mikoa hiyo wamenufaikaje kutokana na mapato hayo?

(c) Je, Serikali inafanya utaratibu gani wa kuwakopesha wakazi hao pembejeo ili walipe baada ya kuuza korosho?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar Saidi Chubi, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, korosho ni zao kuu la biashara katika Mikoa ya Mtwara na Lindi. Mikoa hiyo huzalisha zaidi ya asilimia 70 ya korosho zote zinazozalishwa nchini. Katika miaka 2000/2001 - 2002/2003, Mikoa hiyo ilizalisha jumla ya tani 233,113.

Katika kipindi hicho mikoa hiyo iliuza nje ya nchi takribani tani 228,805 za Korosho zenye thamani ya shilingi bilioni 141.129 ambazo ni sawa na Dola za Marekani 157.86 milioni kwa wastani wa shilingi 895 kwa Dola moja ilivyokuwa katika miaka hiyo; ambazo zilichangia Pato letu la Taifa.

(b) Mheshimiwa Spika, wakazi wa Mikoa hiyo ya Kusini ambao ndiyo wazalishaji wakuu wa zao la Korosho wananufaika na mapato ya mauzo ya Korosho kwa kuwapatia fedha za kutumia kwa ajili ya kukidhi mahitaji yao mbalimbali ya kiuchumi na kijamii ambayo kwa ujumla wake husaidia kupambana na umaskini na kuwaletea wananchi maendeleo katika nyanja mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Spika, wakulima katika ngazi ya familia wameweza kujipatia fedha kwa ajili ya kugharamia mahitaji ya lazima kama vile kununulia chakula, mavazi, kujengea nyumba pamoja na kulipia huduma za lazima zikiwemo karo za shule, matibabu, usafiri na kadhalika.

(ii) Mapato hayo yamewawezesha wakulima kujiendeleza kiuchumi kwa njia ya kukuza kilimo kwa kununulia pembejeo na madawa ya kuulia wadudu kwa lengo la kuongeza uzalishaji.

Aidha, baadhi ya wakulima wametumia mapato hayo kwa kujipatia mitaji ya kuendeshea biashara mbalimbali pamoja na kununulia vitendea kazi na zana nyinginezo kama vile vyombo vya usafiri zikiwemo baiskeli, pikipiki na magari.

(iii) Mapato yatokanayo na ushuru wa mazao yanayokusanywa na Halmashauri za Wilaya yanasaidia katika uboreshaji wa huduma za jamii kama vile ujenzi wa zahanati, shule, barabara na kadhalika ambazo zinawalenga moja kwa moja wakulima Vijijini.

(iv) Fedha za kigeni zitokanazo na mauzo ya Korosho nchi za nje huliwezesha Taifa kununua zana na bidhaa ambazo hazizalishwi hapa nchini kama vile mashine na mitambo, mafuta, madawa na kadhalika. Taifa hutumia zana na bidhaa hizo kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ya wananchi wakiwemo wakulima Vijijini.

(v) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa matumizi ya pembejeo katika kuongeza uzalishaji na ubora wa zao la Korosho imeweka utaratibu wa kuwapatia mikopo ya kununulia pembejeo wakulima wa Korosho kupitia Mfuko wa Pembejeo wa Taifa chini ya Wizara ya Kilimo na Chakula ambao hutengewa fedha kila mwaka.

Kwa mfano, msimu wa mwaka 2002/2003 Serikali ilitenga jumla ya shilingi milioni 440 kwa ajili ya kuwakopesha wakulima kupitia Benki ya *Exim.*

(vi) Aidha, Serikali kupitia Bodi ya Korosho Tanzania, imekuwa ikihimiza kila Wilaya ianzishe Mfuko wa Pembejeo na kuuendesha kwa ufanisi ili uweze kushindana Kibiashara na wafanyabiashara wanaosambaza pembejeo kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo, Mifuko ya Pembejeo inaweza kuwasambazia wanachama wake pembejeo zinazokidhi mahitaji yao kwa wakati muafaka. Serikali pia inawahamasisha na kuwahimiza wakulima kujianzishia Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo *(SACCOS)* vitakavyoweza kuwapatia mikopo ya kununulia pembejeo kwa masharti nafuu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia muda nauliza swali moja tu.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Kwa kuwa tegemeo la wakulima wa korosho ni kupata pembejeo kwa utaratibu unaofaa na kwa kuwa vitendo vya Benki ambayo imepewa dhamana ya kukopeshwa, hiyo *Exim Bank* ni vitendo vyenye ukakasi na vinavyokatisha tamaa wakopaji. Je, kwa nini Serikali tangu mwaka 2002 inasita kuziondoa pesa za Mfuko huu kutoka *Exim Bank* kupeleka *National Microfinance Bank* au kupeleka *Tanzania Investment Bank* au kupeleka Benki ya *CRDB* au Benki zingine zozote zile kama *Rombo Commercial Bank* au za Kilimanjaro za Ushirika na kadhalika? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kwanza utaratibu huu ulitumika baada ya kupata matatizo kwa sisi kukopesha moja kwa moja. Kwa hiyo, tukaona ni vizuri tutumie utaratibu wa Benki. Kwa bahati mbaya waliojitokeza kutufanyia kazi hii ni wachache sana, zilikuwa ni Benki mbili tu ambazo ni *Exim Bank* na *Kilimanjaro Cooperative Bank.* Tumeendelea nao na tukapata matatizo kwa sababu ya uchache wao hawawezi kui-*cover* nchi nzima. Tulilofanya sasa ni kuchukua Benki nyingine na tumechukua Benki ya Wananchi wa Mufindi inayoshirikiana nasi na Benki ya Kagera inashirikiana nasi. Napenda niwahakikishie kwamba, kama kuna Benki Mtwara, tutapenda pia kushirikiana nao. Lakini *National Microfinance Bank* na *Cooperative Bank* na nyingine, hazikujitokeza kushirikiana na sisi katika kazi hii, lakini tuko tayari kushirikiana na *SACCOS* na *SACCAS,* pamoja na Vyama vya Wananchi, kwa mfano, Tunduru tumewatumia kukopesha pembejeo za korosho. *(Makofi)*

Na. 130

**Umiliki wa Ardhi wa Miaka 90**

**MHE. PARSEKO V. KONE (k. n. y. MHE. LEKULE M. LAIZER)** aliuliza:-

Kwa kuwa baadhi ya hatimiliki za ardhi zinatolewa kwa muda mrefu (miaka 90), muda ambao ni mkubwa kuliko umri wa maisha ya mtu ambao unakadiriwa miaka 70 au chini ya hapo: -

(a) Je, kuweka umiliki wa ardhi muda mrefu zaidi ya maisha ya mtu aliyopewa sio kupoteza ushahidi huku hakutakuwa na mtu ambaye ana ushahidi wa eneo hilo?

(b) Je, Makampuni na watu wa nje ambao wanamiliki kwa muda mrefu kama huo ni lini wenye ardhi watatumia ardhi hiyo?

(c) Je, siyo vizuri kwa sasa kupunguza miaka 90 iwe machache kulingana na kushuka kwa maisha ya watu?

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria zilizopo, utoaji wa muda wa miliki za ardhi unategemea mpango wa uendelezaji wa eneo husika. Mpango wa uendelezaji wa eneo unatenga maendelezo katika vipindi vya miaka kwa muda mfupi wa mwaka mmoja mmoja, hadi muda mrefu wa miaka 33, 66 na 99. Haki ya kumiliki ardhi hutolewa kwa maandishi ambayo yamo katika hati ambazo hutunzwa katika Ofisi za Serikali, zenye usalama wa hali ya juu na pia nakala zake hutunzwa na wamilikaji.

Umilikishaji ardhi wa muda mrefu zaidi ya maisha ya mtu hauwezi kuwa sababu ya kupoteza ushahidi wa umilikaji hata kama watu wote waliokuwa hai wakati miliki ilipotolewa watakuwa wamefariki dunia. Ushahidi utaendelea kuwepo kutokana na kuwepo na kumbukumbu sahihi za wamiliki wa ardhi nchini, kuwepo na ushahidi wa kukalia na kutumia ardhi na kuwepo kwa ushahidi wa simulizi za mapokeo katika sehemu husika.

(b) Mheshimiwa Spika, Makampuni na watu wa nje na ndani ya nchi waliopewa haki ya kumiliki ardhi kwa muda mrefu katika baadhi ya maeneo nchini, kisheria wataendelea kuitumia ardhi hiyo kwa muda wote uliotolewa katika miliki yao. Haki ya kumiliki ardhi hiyo inaweza kufutwa endapo itathibitika kuwa wamiliki wamevunja masharti ya umilikaji yaliyotolewa katika hati ya kumiliki ardhi. Aidha, Halmashauri ya Jiji, Manispaa, Miji na Wilaya kwa kushirikiana na Mikoa, zinaweza kuleta Wizarani kwangu mapendekezo ya kufuta miliki za ardhi katika maeneo yao wanapoona inafaa kwa maslahi ya umma.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali haina mpango wa kupunguza muda wa kutoa haki za kumiliki ardhi kutoka miaka 99 kuwa miaka machache kutokana na sababu zifuatazo: -

(i) Umri wa mtu siyo kigezo kinachozingatiwa katika kutoa muda wa miliki. Kigezo muhimu ni masharti ya uendelezaji yanayoandamana na aina ya mradi unaotekelezwa;

(ii) Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 kifungu cha 4(3), haki ya kumiliki ardhi inatambuliwa kama mali. Kwa msingi huo inaweza ikarithishwa kwa mrithi pale mmiliki anapofariki;

(iii) Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 kifungu cha 22(1)(e), kinampa Kamishna wa Ardhi mamlaka ya kutoa ardhi kwa miliki ya muda wowote usiozidi miaka 99; na

(iv) Hata pale miliki inapotolewa kwa muda wa chini ya miaka 99, muda huo unapomalizika na ikadhihirika kuwa maendelezo yaliyopo katika ardhi yanaweza kudumu kwa miaka mingine kadhaa, Serikali huwaongezea muda wahusika. *(Makofi)*

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, Waziri anaweza kutueleza ni vikao gani vinavyopendekeza kwamba mmiliki wa ardhi amekiuka masharti ili Waziri aweze kumfutia hati hiyo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, vikao vinavyohusika hatua ya mwanzo kabisa ni Kamati za Kugawa Ardhi, ambazo zipo katika Halmashauri zote. Kwa hiyo, ningeomba Kamati hizo ziweze kufuatilia uendelezaji wa maeneo yote ambayo wameyagawa kwa wamilikaji mbalimbali. Yale ambayo hayaendelezwi basi haraka waweze kukaa na kutoa mapendekezo kwa hatua ambazo ni za kisheria, kuweza kubatilisha miliki za maeneo hayo. Hatua ni kwamba, zinaanzia kwenye Halmashauri wanatoa mapendekezo yanakuja Wizarani na Wizarani ndiyo tunahitimisha hatua za mwisho katika utaratibu wa kubatilisha hatimiliki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha tunaendelea na matangazo ya vikao vya leo kama ifuatavyo: Kuna Kamati tatu ambazo zimepangiwa kufanya vikao vyake leo. Kamati ya kwanza ni ya Maendeleo ya Jamii, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Sophia Simba, anaomba Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, wakutane leo tarehe 23 kuanzia saa 5.00 asubuhi, chumba namba 227. Kamati ya pili ni ya Uwekezaji na Biashara, Mwenyekiti wake Mheshimiwa William Shellukindo, anaomba Wajumbe wa Kamati hii wakutane leo saa 5.00 asubuhi hii, chumba namba 231 ghorofa ya pili. Kamati ya tatu ni ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Beatus Magayane, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo ya *LAAC* wakutane chumba namba 133 mara baada ya kipindi cha maswali.

Taarifa nyingine inatoka kwa Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake *(TWPG),* Mheshimiwa Janeth Mashele, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, leo tarehe 23 Aprili, 2004, kuanzia saa 1.00 jioni kutakuwa na tafrija itakayofanyika katika Viwanja vya Bunge. Kadi za mwaliko

zimetolewa kwa Wabunge wote, lakini kama kuna Mheshimiwa Mbunge yeyote ambaye hajapata kadi, ahesabu kwamba anakaribishwa kwenye tafrija hiyo. *(Makofi)*

Tangazo lingine ni kwamba, hotuba au hoja ya kufunga Mkutano huu wa 15 wa Bunge itatolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuanzia saa 11.00 jioni na kama tunavyojua, Redio Tanzania Dar es Salaam, huwa inatangaza Hotuba ya Waziri Mkuu moja kwa moja. Kwa hiyo, endapo tutamaliza yaliyopo kwenye *Order Paper* kabla ya saa 7.00 mchana, shughuli zitasitishwa mpaka saa 11.00.

Mwisho wa matangazo. Katibu, tuendelee na *Order Paper.*

**KAULI ZA MAWAZIRI**

**Tamko la Serikali Kuhusu Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Mchuchuma**

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa tamko la Serikali kuhusu Mradi wa Mchuchuma wa kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kuwa, katika Kikao cha 14 cha Bunge, kilichofanyika Februari, 2004, Serikali iliahidi kutoa tamko ambalo lingefafanua mkakati wa kuendeleza mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe ya Mchuchuma. Mradi huu unadhaminiwa na kundi la wawekezaji likiongozwa na Kampuni ya *Siemens* na linahusisha Shirika letu la *NBC.* Kwa hiyo, mazungumzo ya awali kuhusu Mradi wa Mchuchuma yamehusisha wawekezaji kwa upande mmoja na Serikali kwa upande wa pili. Upande wa Serikali umeongozwa na Wizara ya Nishati na Madini na umeshirikisha *TANESCO*, Kamati za Mawaziri, Makatibu Wakuu na Wataalam pia wa *Mtwara Development Corridor.*

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Mchuchuma una umuhimu mkubwa kwa Taifa letu. Mradi wa kuzalisha umeme kutokana na makaa ya mawe kama vile Mradi wa Gesi ya Songosongo na Mradi wa Gesi ya *Mnazi Bay,* yote ina madhumuni ya kuzalisha nishati kutokana na raslimali zetu nchini na kupunguza kuitegemea *TANESCO* kwa sasa kwenye vyanzo vya maji na mafuta ambavyo haviaminiki au ni ghali kifedha, miradi ya kuzalisha umeme ya Sekta binafsi ni muhimu sana. Wakati Mradi wa *Songas* utakapoanza baadaye mwaka huu wa 2004, pamoja na Mradi wa *IPTL,* ambao sasa hivi unafanya kazi, itakuwa miradi hii miwili inachangia zaidi ya *megawatts* 200 katika gridi ya Taifa. Hata hivyo, miradi ya umeme inahitaji uangalifu mkubwa ili kuliepusha Taifa na matatizo yaliyojitokeza katika Mradi wa *IPTL,* ambayo yameisababishia Serikali kubeba mzigo mkubwa wa kifedha.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, mradi wa kuzalisha umeme wa Mchuchuma lazima uzingatie mambo mengi ikiwa ni pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji wa mradi, ushindani wa vyanzo vingine vya umeme vyenye bei nafuu, kupunguza bei ya umeme kwa *TANESCO* na kwa watumiaji, kufanyia uchunguzi wa kutosha kwenye

maeneo kama kuna athari za mazingira na kuunganisha kituo cha umeme kitakachojengwa cha Mchuchuma *(Power House)* na gridi ya Taifa na kutokuibebesha Serikali sehemu kubwa za gharama za mradi *(Market Risk),* kupitia Mkataba wa Ununuzi *(Power Purchase Agreement),* ikilinganishwa na wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeridhika kuwa wawekezaji wa mradi wa Mchuchuma lazima wafanye marekebisho niliyoyataja ili mradi uwe endelevu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi mbalimbali na hali halisi ya Sekta ya Nishati hapa nchini, hasa ukame uliokithiri, uendeshaji wa mitambo ya kuzalisha umeme, kutumia mafuta na ununuzi wa umeme wa *IPTL,* Mradi wa Umeme wa Mchuchuma unaweza kutekelezwa kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kwamba, Wizara ya Nishati na Madini iharakishe majadiliano na wawekezaji wa Mradi wa Mchuchuma ili waufanyie marekebisho ya upeo, taratibu za utekelezaji na gharama za Mradi ili umeme utakaozalishwa uweze kutumika bila kuongeza bei za umeme kwa watumiaji au Serikali kuwajibika kulipa malipo stahili kwa wawekezaji endapo *TANESCO* watashindwa kuyamudu kama ilivyo wakati huu kwenye Mradi wa *IPTL.* Baada ya marekebisho hayo, Wizara ya Nishati na Madini ishughulikie Mikataba ya Mradi kwa kuzishirikisha kikamilifu, Asasi husika za Serikali kwa kuzingatia maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefikia maamuzi haya ya msingi kwa kutambua mchango wa Sekta ya Nishati katika kuimarisha uchumi wa nchi kwa misingi iliyo endelevu. Lengo la Serikali ni kutumia vyanzo asilia vya nishati vilivyopo nchini, kuepuka kutegemea maji kama chanzo pekee na kuwa na umeme wa uhakika kuchochea ukuaji wa uchumi na kuharakisha maendeleo ya Wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa Mchuchuma kama ilivyoelezwa hapo awali utafungua ukurasa mpya katika historia ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

Muswada wa Sheria ya Bandari wa Mwaka 2004 *(The Ports Bill, 2004).*

Muswada wa sheria ya Kurekebisha Sheria za Uchaguzi wa Mwaka 2004 *(The Electoral Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2004).*

Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2004 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill 2004).*

*(Miswada iliyotajwa hapo juu ilisomwa Bungeni*

*kwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Miswada hii tumewagawia wote leo hii na kwa utaratibu uliopo ni kwamba, inasomwa mara ya kwanza tu, lakini itajadiliwa katika mkutano wa baadaye. Tunawaomba muitunze Miswada hii, muisome kwa uangalifu ili kujiweka tayari kwa mjadala wakati wake utakapowadia.

Tunaendelea na *Order Paper,* Katibu.

**Muswada wa Sheria ya Kodi ya Mapato wa Mwaka 2004**
***(The Income Tax Bill, 2004)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*
*(Majadiliano yanaendelea)*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. IDDI M. SIMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii na kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa juhudi zake za kuzingatia mawazo ya wadau na Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge, ningependa kutoa maoni yafuatayo: -

Kwanza, kwa kuzingatia umuhimu wa Muswada huu na jinsi unavyogusa maisha ya Wananchi na ugumu wa kuelewa vipengele vyake, ingefaa utolewe muda wa mazungumzo ya ziada ya wadau na Kamati ya Fedha. Kwa jinsi ulivyo, Muswada bado una vipengele vinavyogongana na kutoeleweka. Havitambui uwezo mdogo wa walipakodi wa kuelewa namna wanavyotakiwa kutimiza wajibu wao na kudai haki zao chini ya sheria inayokusudiwa. Kwa sababu Muswada bado unachanganya na una makosa mengi ya uandishi, utawapa shida walipaji na wakusanyaji wa kodi na hatimaye kupotosha madhumuni ya Sera.

Pili, ukusanyaji wa kodi unakuwa na maana pale tu unapowagusa watu wote wanaostahili kulipa kodi na pale kodi inayokusanywa inapotumiwa kwa maendeleo ya watu kwa maana hii ingefaa: -

(a) Wigo wa kodi uwe mpana zaidi. Hivi sasa inakadiriwa kwamba, wafanyakazi wa kuajiriwa na wa kujiajiri wanafika milioni 15, lakini wanaoguswa na mfumo wa kodi ni milioni mbili tu. Hali hii inatokana na mfumo wa kodi ulioanzishwa mwaka 1929 na Serikali ya Kikoloni na kurekebishwa kwa nyakati mbalimbali, katika utaratibu wa kuwaweka kando Wananchi wanaojishughulisha kwenye Sekta isiyo rasmi *(Informal Sector).* Utawala wa Kikoloni haukuwatambua Wananchi kama walipakodi muhimu. Kwa hiyo, walipuuzwa na Sheria za Kodi ziliwaacha nje ya wigo kwa nyakati zote palipotokea mabadiliko ya sheria hizo. Matokeo yake ni kwamba, maendeleo yote ya kiuchumi na shughuli za kisasa za uzalishaji mali na biashara kubwa ziliendeshwa katika Sekta ambayo haikuhusisha umma wa Wananchi. Hii ndiyo hali iliyopo sasa yaani Sekta ndogo rasmi inayoendesha shughuli kubwa kwa teknolojia ya kisasa inayojumuisha waajiri na waajiriwa wapatao milioni mbili tu kwa upande mmoja na Sekta isiyo rasmi

inayoendesha shughuli za uchumi kwa nyenzo za jadi inayojumuisha watu milioni 13 wasiojulikana *(Informal Sector).* Ili kupanua wigo ni lazima kupanga utaratibu wa kuwaendeleza na kuwaingiza Wananchi walio wengi wakiwemo wakulima, wafugaji, wavuvi, mafundi na wafanyabiashara ndogo ndogo katika Sekta rasmi itakayotambuliwa.

(b) Sheria ya Uwezeshwaji iletwe Bungeni haraka. Ikizingatiwa kwamba, baada ya miaka michache Tanzania itakuwa katika soko la pamoja na nchi za Afrika Mashariki na za Kusini na ikizingatiwa vile vile kwamba, ndani ya miongo miwili dunia nzima itakuwa soko la pamoja, ni lazima hivi sasa Taifa liwe na mipango ya kuwaandaa Wananchi wa Tanzania kwa mashindano ya kibiashara na nchi zingine. Hili ni suala la uzalishaji mali kwa mtindo wa kisasa na utakaojumuisha Sekta zote za uchumi kwa kutumia raslimali za Taifa. Raslimali za Taifa ni pamoja na Wananchi wake ambao wanahitaji mafunzo na uwezeshwaji kifedha na kupewa fursa za upendeleo katika shughuli mbalimbali za umma. Ifahamike kwamba, Wananchi wataalam, mabingwa, katika fani zote kama vile wanasheria, wahasibu, wahandisi na kadhalika, wanashindana kwa tabu sana na wataalam wa nje. Mashindano hayo yatakuwa magumu zaidi kadri siku zinavyosogelea ushirikiano rasmi wa Kimataifa na utandawazi. Hali hii inawagusa hata wananchi wasioelimika na wanaojishughulisha na kazi duni mijini na vijijini.

Mfumo wa kodi ni lazima utumiwe kama chombo cha kuhamasisha Taasisi na Makampuni yatakayoshirikishwa katika mipango ya kuandaa umma wa Wananchi ili kuipa Tanzania uwezo wa kuingia ipasavyo katika soko la dunia. Inafahamika kwamba, hivi sasa Mabenki yetu pamoja na Taasisi za Fedha, yana ukwasi mkubwa mno. Hizi ni amana za Wananchi ambazo kwa utaratibu wa leo na mfumo huu wa kodi hazitumiki kwa maendeleo ya watu. Sheria ya Uwezeshwaji inaweza kufungua njia.

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Naibu Waziri wa Fedha, Makatibu Wakuu, Wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha na wa Mamlaka ya Kodi, kwa kazi nzuri wanayofanya. Aidha, ninaunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja.

Pamoja na kuunga mkono hoja hii, ninaomba yafuatayo yazingatiwe: -

(i) Wizara na Mamlaka watoe elimu ya kutosha kwa Wananchi kuhusu Sheria mpya ili kila mwananchi ajue anatakiwa kufanya nini (wajibu) na ana haki gani kutokana na sheria hii;

(ii) Mamlaka ijenge hali ya urafiki na mlipakodi na iondoe hali ya kumwona mtoza kodi kuwa ni adui, mla rushwa na mwenye nia ya kumwumiza mlipa kodi. Hivyo, kutokana na *self assessment,* mlipa kodi anayejikadiria vyema kodi yake apewe motisha kwa kupunguziwa kiasi cha kodi anachotakiwa kulipa; na

(iii) Nchi nzima inufaike kwa kodi inayokusanywa. Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, leo hii (21 Aprili, 2004), alipokuwa akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa barabara ya lami kutoka Dodoma kwenda Manyoni, alisisitiza juu ya wajibu

wa Wananchi kulipa kodi ili kuipa Serikali uwezo wa kutimiza wajibu wake ikiwa ni pamoja na kujenga barabara. Lakini pamoja na kwamba, Wananchi wote kwa namna moja au nyingine wanalipa kodi, matunda ya kodi hizo yanaelekezwa kwenye maeneo fulani ya nchi na kuacha maeneo mengine yakiwa hayana maendeleo na kukosa miundombinu muhimu hasa barabara za lami na umeme ambavyo havipo Mkoani Kigoma. Wananchi wote kama walipakodi wanastahili kufaidi matunda ya kodi walipazo.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. SHAMSA S. MWANGUNGA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Waziri wa Fedha na timu yake yote, kwa kazi nzuri na yakinifu ya Muswada huu. Ninaunga mkono Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchangia yafuatayo ili kuuboresha muswada huu:-

(a) *Paragraph* ya 3 katika madhumuni imeongelewa kuhusu *self assessment* ya *taxpayers*. Lakini hakuna popote ilipoelezwa kwa kirefu kuhusu hiyo *self assessment* itakuwaje. Hii ni sehemu muhimu sana kwani hata nchi zilizoendelea ulimwenguni mtindo huo unatumika. Ingefaa hii ifafanuliwe vizuri.

(b) *Part (v)* katika madhumuni, kampuni za uchimbaji madini hazikutajwa na ambapo zina mchango mkubwa sana.

(c) *Section 15,* kifungu cha pili, kuhusu kuhifadhi mazingira, imeongelewa tu kuhusu kilimo kwani fani zingine hazikuongelewa jinsi teknolojia ya kulinda mazingira itakavyokuwa. Pia kwa nini kusiwepo kodi ya uchafuzi wa mazingira kama nchi zingine wanavyotoza, viwanda au kampuni zinazoharibu au kuchafua mazingira mfano, *plastic bags,* viwanda vya kuchimba madini na kadhalika.

(d) *Section 13* na *16* kuhusu *trading stock*, haya ni masuala ya kihasibu na yana *standard* zake. Ziko za *international* pia na tunazo zetu za *national,* ambazo zinasimamiwa na *NBAA.* Ningetoa ushauri ya kwamba, haya yote yangeachwa yashughulikiwe na yafuate *accounting standard* badala ya kuhusishwa na kodi, *otherwise* italeta *friction* katika utekelezaji.

(e) Viwanda na makampuni madogo yahamasishwe kwa kupewa *capital allowance.* Kwa hiyo, sheria hiii iwe na mwelekeo wa kusaidia viwanda na kampuni ndogo ili ziweze kuachangia kikamilifu katika Pato la Taifa.

**MHE. DR. AMAN W. A. KABOUROU:** Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu na Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kwa nyadhifa zao muhimu za Kimataifa kwa niaba ya Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, napenda pia niseme hapa kuwa, naunga mkono sheria hi. Hata hivyo, nina wasiwasi mkubwa kuhusu ufafanuzi wa sheria hii katika siku zijazo. Kwa mfano, tatizo kubwa tulilonalo sasa ni ufinyu wa makusanyo na hivyo kushindwa kutekeleza miradi yetu ya maendeleo Kitaifa. Kiakili tu, ni kuwa kama kipato chetu kingeongezeka, basi mengi tunayoyakosa leo kama vile huduma za jamii, maji, afya, miundombinu na kadhalika tusingevikosa. Lakini tukijiuliza swali la msingi, je, *TRA* kwa sasa inakusanya kiasi gani cha kile ambacho tungeweza kukusanya? Nielewavyo mimi kwa sasa *TRA* imekusanya si zaidi ya asilimia 15 ya pato la kodi litokanalo na Pato la Taifa. Sasa tujiulize, je, *TRA* yenyewe ni chombo sahihi kwa ukusanyaji wa kodi yetu au kuna haja ya kubinafsisha shughuli ya ukusanyaji kodi kwa niaba ya Taifa letu. Katika hili sidhani kuwa kuna sababu ya Watanzania kuwa na wasiwasi wowote, kwani tayari tumekwisha jifunza kutokana na kumbukumbu zetu za ukusanyaji wa kodi katika Halmashauri zetu hapa nchini baada ya Halmashauri hizo kubinafsisha shughuli hii. Kwa mantiki hiyo, inahusiana na Kamati ya Fedha na Uchumi inaposhauri kuwepo na programu ya muda mfupi na mrefu na hata sheria ya kufuatilia ufanisi wa barua hii ili baada ya muda muafaka tuweze kufanya mabadiliko ambayo ikibidi yawe ni kukubali ubinafsishaji.

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kuungana na Wabunge wenzangu kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, kwa maandalizi na uwasilishwaji mzuri wa Muswada huu. Wote tunafahamu utendaji wake tangu zamani na kwamba Muswada huu, umewasilishwa wakati muafaka. Aidha, nampongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, ambaye ameonyesha uwezo mzuri na uaminifu mkubwa katika kushughulikia masuala mbalimbali ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Ndugu Grey Mgonja, Ndugu Lyimo na Ndugu Nyachia, kwa kazi zao nzuri. Aidha, ninampongeza kwa dhati Kamishna Mkuu wa *TRA,* kwa kazi nzuri sana anayoifanya. Kwa kweli ameonyesha mfano mzuri sana katika suala zima la ukusanyaji ya mapato ya Serikali. Aidha, ninawapongeza Wabunge wenzetu kwa kuchaguliwa kwao kushika nafasi mbalimbali katika nyanja za Kimataifa. Nasi tunawatakia kila lenye kheri katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ningependa nirudi kwenye Muswada. Sheria hii imeletwa wakati muafaka na ilikuwa ni lazima Muswada huu uje, kwa sababu mazingira yaliyotungiwa sheria hii wakati huo yamekamilika. Hivyo, tunataka huu mfumo wa sasa wa kodi uchochee kukua na kupanuka kwa uchumi. Pia tunataka kodi iache mapato ya kutosha kwa wananchi ili waweze kujiwekea akiba ambayo wataitumia kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hii ninapendekeza kuwa si vizuri kuendelea kuwatoza kodi wafanyakazi kwa mbinu za kuwaongezea viwango vya kodi au kuwaongezea njia mbalimbali za kuwatoza kodi watu wale wale. Hapa nashauri itafutwe mbinu nyingine ya kupanua wigo wa kodi kwa kuwaingiza wapya kama Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wa Kamati hii walivyobainisha.

Serikali ifanye mkakati wa makusudi wa kuwasaidia wafanya biashara ndogo ndogo wote nchini ambao ni wengi, kuwakopesha kwa masharti nafuu, kuwapa ujuzi kwa njia ya mafunzo, kuwasaidia kuwatafutia masoko, ili hatimaye waweze kuongeza kipato chao ambacho kitawasaidia kuwa walipa kodi baadaye. Serikali ihakikishe misamaha ya kodi haitolewi bila kuwepo sababu za msingi. Njia hii itasaidia pia kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali iwasaidie wawekezaji wa ndani katika kukuza Sekta ya Viwanda. Hasa wazalendo wapewe kila aina ya msaada watakapokuwa wamefanikiwa watakuwa walipa kodi wazuri. Aidha, Serikali iweke mkakati wa makusudi wa kulinda bidhaa za ndani. Serikali pia iweke mazingira mazuri ambayo yatazidi kuwavutia wawekezaji wa nje kama inavyofanya sasa kwa kupunguza urasimu ambao unaweza ukawakatisha tamaa wawekezaji. Serikali kwa makusudi iisaidie Sekta ya Kilimo. Maana uchumi wa mtu mmoja mmoja ukipanuka hata maeneo ya kutoa kodi yataongezeka. Aidha, Serikali iwape upendeleo maalum wawekezaji wanaotaka kuja kuwekeza katika sekta ya kilimo.

Ninamwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uongozi mzima wa *TRA,* kuhakikisha kwamba, wakadiriaji wa kodi wanatenda haki kwa malipa kodi. Maana wakadiriaji wawe wana madaraka makubwa, wakiyatumia vibaya Wananchi wataumia, watatafuta mbinu za kukwepa kulipa kodi na tutajenga mazingira ya vishawishi vya rushwa. Hivyo, wale watakaobainika kwenda kinyume na maadili ya kazi zao, basi wachukuliwe hatua kali ili iwe fundisho kwa wengine. Sijui katika eneo hili wangapi wameshawajibishwa ili iwe ni fundisho kwa wengine?

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Naunga mkono hoja kwa asilimia 100. Napenda kushauri kuwa kodi ni muhimu sana na mlipakodi kwa Serikali ni mteja muhimu sana. Lazima Serikali ielewe kuwa kufilisika ama kumfilisi mlipakodi ni kupungukiwa walipakodi. Kama Serikali inaweza kumwendeleza mlipa kodi ni vizuri sana. Ninaomba kushauri kuwa, wapo wafanyabiashara ambao wanadaiwa na Serikali lakini wanadai Mashirika yaliyoko *PSRC* ama *LART,* sasa je, Serikali *(TRA)* itawafanya nini hawa, wengine walikopa kwenye Mabenki ili wafanye biashara na kuweka dhamana nyumba zao kwenye Mabenki na wengi nyumba hizo zimenadiwa?

Mheshimiwa Spika, ni vyema wafanyabiashara hawa wakawekewa utaratibu mzuri wa kuendelea kuwadai hawa kwa utaratibu wa kuwawezesha kulipa madeni ya namna hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PHILIP A. MAGANI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja na kumpongeza Waziri wa Fedha na wasaidizi wake pamoja na Wataalam wa Wizara ya Fedha na Watendajii wa *TRA.*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa vile Muswada kama ulivyoletwa awali ulikuwa na vipengele vingi ambavyo kama vingebaki katika Muswada, vingeleta kero kubwa kwa Wananchi walipakodi. Lakini kwa kuzingatia ushauri wa Kamati ya Fedha na Uchumi, pamoja na wadau wengine, maudhui ya Muswada huu yameboreka sana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, napenda kutoa mchango wangu katika suala la wigo wa mlipakodi ambalo hata Mheshimiwa Waziri amekiri kuwa mpaka sasa umekuwa finyu sana. Hili ni eneo ambalo linafaa kuzingatiwa wakati wa kutekeleza sheria hii. Wakwepaji wa kodi ni wengi hususan wafanyabiashara wakubwa, ambao wenzetu hawawi wazi katika kuelezea mapato yao. Hawa ni lazima washughulikiwe na si lazima kwa kuwa wakali bali kwa kuelimisha na kujenga mahusiano yanayojenga imani na kuaminiana kati ya matajiri hao na watoza kodi.

Mheshimiwa Spika, Tanzania asilimia 80 ni wakulima na hawa ni wakulima wadogo ambao uwezo wao wa kuzalisha ni mdogo na hawana uwezo wa kuongeza mazao yao kwa vile hawana uwezo wa kukopa kutoka katika Taasisi zetu za fedha, ambazo wanang'ang'ania masharti ambayo kwa vyovyote vile hayawezi kuhitimishwa na wakopaji hao. Taasisi za Fedha ziende kwa wakulima badala ya kungoja maofisini wakisubiri wakopaji wadogo pamoja na wakulima waende katika maofisi hayo. Maofisi yako mbali, pamoja na ukosefu wa uelewa, hawana uwezo wa kufika huko. Hawa wakiwezeshwa kwa kupatiwa mikopo ya kuongeza uzalishaji, siyo tu kwa kuongeza kipato chao bali pia kufikia viwango ambavyo vitawezesha kuingia katika wigo huo, ili mradi tu wanawekewa utaratibu wa kulipa kama inavyoelezwa kwa utaratibu wa *self assessment,* utaratibu ambao utahitaji elimu kwa wahusika. *TRA* lazima ijiandae kwa hili.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo napenda kuchangia ni ule utaratibu unaotumika na *TRA* katika makadirio ya kodi kwa kuzingatia umaarufu wa eneo ambapo biashara hufanywa. Kwa mfano, wafanyabiashara wadogo ambao wapo katikati ya Jiji la Dar es Salaam ni lazima walipe kiwango cha Sh.1,000,000/= bila kujali kipato chake ni kiasi gani. Wengi wa wafanyabiashara hawa ni wadogo na pengine wameweza kupata mahala pa kufanyia kazi tu kwa vile kodi za pango ya nyumba za *National Housing Corporation* ni nafuu na siyo kuwa wao wana kipato cha juu. Kwa kuzingatia hili, natoa rai kwa *TRA* kwamba, katika kukadiria kodi ya wafanyabiashara hawa wadogo ambao sehemu zao za kufanyia kazi zipo katikati ya Jiji, watozwe kodi kwa kuzingatia pato lao na siyo *location* ya ofisi zao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Fedha.

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil P. Mramba, Naibu Waziri wake na timu nzima ya utalaam na utendaji, ikiongozwa na Katibu Mkuu, kwa kuleta Muswada huu wa Sheria ya Kodi ya Mapato. Tangu Wizara iwekwe chini ya Uongozi wa sasa na Mheshimiwa Rais, jamii nzima ya Tanzania, imeona maendeleo ya uchumi ambayo hayakuwahi kutokea. Matumaini ya Mtanzania yameinuliwa. Wizara ya Fedha kupitia kwa Waziri wa Fedha, inastahili pongezi na tuzo za pekee sana.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Kodi ya Mapato ni sehemu muhimu ya juhudi za Wizara za kuweka misingi ya maendeleo ya uchumi ndani ya utandawazi unaohitaji *strong government.*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchangia kama ifuatavyo: Kwanza kabisa, naunga mkono hoja. Pili, wachangiaji wengi wamesisitiza umuhimu wa elimu kwa Wananchi hususan kuhusiana na suala la *self assessment.* Katika hili napendekeza elimu kwa Wananchi ijenge dhana kwamba, kulipa kodi ni heshima, ni utu na ni demokrasia.

Mheshimiwa Spika, elimu ya kodi ifundishwe kwenye ngazi zote za elimu *(Formal Education),* kuanzia shule ya msingi. Hii ndiyo njia pekee ya kujenga dhana ya kulipa kodi, ni heshima na itahakikisha *speed* ya ku-*institutionalize self assessment* endelevu.

Mheshimiwa Spika kupanua *tax base* itabidi iambatane na sera madhubuti ya kuongeza uwezo wa kulipa kodi. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. FATMA SAID ALI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nampongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, kwa marekebisho makubwa waliyoyafanya kwenye Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, nina maswali yafuatayo:-

(a) Tutafanyaje biashara kwa nchi zetu tatu yaani Kenya, Uganda na Tanzania ikiwa Sheria ya Kodi ya Mapato kwa nchi hizi tatu za Afrika Mashariki ziko tofauti?

(b) Sheria hii ya Kodi ya Mapato haitaathiri kwa kuwa na ushuru wa pamoja *(Custom Union)* katika nchi zetu za Afrika Mashariki?

(c) Je, Serikali imefanya utafiti wowote kuangalia misingi ya utozaji kodi, viwango vya kodi na wale wanaostahili kulipa kodi katika nchi zetu za Afrika Mashariki?

(d) Je, Mtanzania mwanamama, mfanyabiashara ndogo ndogo mfano, Mama Ntilie au mtengenezaji batiki, amepewa jukumu la kujikadiria mwenyewe kulipa kiwango cha kodi ataweza kufanya hivyo?

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kuwa, kuwepo na semina mbalimbali kwa wadau wote pamoja na Zanzibar.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa, Mheshimiwa Basil P. Mramba, Waziri wa Fedha, kwa kuleta Muswada wa Sheria ya Kodi ya Mapato wa mwaka 2004. Muswada huu umeletwa wakati mzuri, ambapo Serikali inashawishi uwekezaji kutoka nje ya nchi na ndani, maana eneo la kodi mbalimbali za mapato ni moja ya

masuala ambayo yamekuwa yakipigiwa kelele. Muswada huu ni wa mapinduzi katika shughuli za utozaji kodi hapa nchini. Hongera sana. Aidha, nawapongeza Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Makatibu Wakuu na Watendaji wengine, kwa kumsaidia Waziri kwa ufanisi mkubwa na kumuwezesha kuwasilisha Muswada mzuri na wenye mwelekeo makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Pili, kati ya *formal sector* na *informal sector* ina utata mkubwa. *Informal sector* ni kubwa sana lakini hailipi kodi na *formal sector* ni ndogo na ndiyo inayolipa kodi. Hata ndani ya *formal sector* kuna wawekezaji wajanja ambao sehemu kubwa hawalipi kodi. Sababu wanazotoa siyo rasmi eti wamechangia Chama Tawala, wawekezaji hao ni hatari wanaharibu uchumi wa nchi. Wapo pia wafanyabiashara wanaoweka vitabu viwili vya *accounts*, zile zenye kodi na zile zisizolipia kodi. Wanadiriki hata kumwuliza mteja eti anataka bei yenye kodi au isiyo na kodi!

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unaelekea kwenye kupanua wigo. Vijana wetu watoza ushuru wawe na imani na ajira hii wasikubali kununuliwa na wawekezaji na wafanyabiashara wajanja.

Tatu, mitumba ya magari na bidhaa mbadala itozwe kodi kubwa kuliko mpya ili tupunguze kuifanya nchi yetu kuwa jalala.

Nne, suala la *tax exemption* ya wahisani nakuomba ulifanyie kazi hasa katika *International Forum* hasa katika vikao vya *World Bank and IMF* na Kamati zao na hata katika vikao vya *UN,* kwanza, tufanye utafiti ni kiasi gani tunapoteza licha ya mradi na mishahara ya watalaam wao. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama alivyowatangazia Mheshimiwa Naibu Spika jana jioni, wasemaji wote waliojiandikisha kuchangia Muswada huu wamemalizika, wote wamechangia. Kwa hiyo, sasa ni zamu ya watoa hoja kuhitimisha hoja yao, naanza na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nami nitoe mchango wangu kwa hoja ya Waziri wa Fedha, kuhusu Muswada wa Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa mchango wangu, naomba pia niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu na Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kwa kuteuliwa ama kuchaguliwa kuwa Marais katika maeneo tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hoja mbalimbali zilitolewa na Waheshimiwa Wabunge na nitatoa ufafanuzi ama maelezo kwa baadhi ya hoja na Mheshimiwa mtoa hoja atamalizia zile nyingine ambazo nitakuwa sijazigusia.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza iliyotolewa ni kuhusu masharti ya mtu kupatiwa unafuu wa gharama za uchakavu yabadilishwe. Badala ya mwenye biashara kumiliki na kutumia raslimali husika, itakiwe ama kumiliki au kutumia raslimali hiyo.

Mheshimiwa Spika, masharti ya kupatiwa unafuu wa gharama za uchakavu huwa ni matatu. Kwanza, kuingia gharama, pili, kumiliki raslimali husika na tatu ni kutumia katika kuzalishia mapato yanayotozwa kodi.

Mheshimiwa Spika, tukitumia ushauri wa Mheshimiwa Nimrod Mkono, kuna athari zifuatazo: Kwanza, tutatoa unafuu kwa mitambo ambayo haizalishi mapato na pili, tunaweza kutoa unafuu kwa anayemiliki na anayetumia raslimali husika mara mbili na mwisho ni kinyume na taratibu za kawaida za kiuhasibu za *depreciation.*

Hoja ya pili ni kwamba, iwapo mpangaji ataingia gharama kuhusiana na nyumba anayopanga, gharama hizo ziruhusiwe kama *depreciation* katika mwaka huo huo *(100 percent expensing).*

Mheshimiwa Spika, kanuni za msingi wa kutoa gharama zimeainishwa katika kifungu cha 11(2) na kifungu cha 11(3). Gharama za kawaida za mpangaji zinaweza kuingizwa hapo. Pili, iwapo gharama zinahusu mali ya kudumu lakini si sehemu ya jengo alilopanga *(Temporary Partition),* raslimali inayopatikana ni *fixtures and fittings* na kupata punguzo la asilimia 121/2 kwa mwaka. *Fixtures and fittings* ni sehemu ya *Class 3* ukurasa 135 wa Muswada.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu inahusu mapato ya ubia *(partnership),* yakokotolewe yaani kwamba ubia unatozwa kodi na kisha kugawiwa kwa wabia. Hivi ndivyo ilivyo katika Muswada na ni kwa mujibu wa kanuni na misingi ya kiuhasibu. Hata hivyo, katika kukokotoa mapato ya ubia, malipo yoyote kwa wabia hayapunguzwi kama gharama kwa kuwa ni sehemu ya mgawanyo wa faida.

Mheshimiwa Spika, ilitolewa hoja pia kwamba, mishahara na posho zinazolipwa na wabia kutoka katika ubia ipunguzwe kama gharama wakati wa kukokotoa faida ya ubia na pia kulikuwa na hoja kwamba, mapato ya mbia kutokana na mshahara na posho kwa upande mmoja na mgao wa faida kwa upande mwingine, yatozwe kodi pasipo kuunganishwa.

Mheshimiwa Spika, maelezo kwa hoja hizi mbili ni kwamba, kwa kuwa ubia hautozwi kodi kwa peke yake, hakuna umuhimu wa kutoa mishahara na posho kwa wabia kabla ya kujua faida ya biashara ya ubia huo. Mishahara na posho ni sehemu ya mgao wa faida hiyo kwa wabia husika. Ikumbukwe kwamba, wabia siyo waajiriwa wa ubia.

Pili, kwa msingi huo mshahara na posho kwa mbia haiwezi kuwa mapato yatokanayo na ajira. Aidha, misingi ya kiuhasibu nayo inaendana na msimamo huu. Kwa hiyo, kitendo hiki ni kugawa mapato yatokanayo na biashara kwenye vianzio viwili kwa nia ya kupunguza kiasi cha kodi. Hata hivyo, uwezekano wa kutenganisha mishahara na mgao wa faida utaangaliwa katika kupitia sheria ya ubia ili kuangalia uwezekano wa sheria kuruhusu *limited liability partnership.*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba, walipakodi walioajiriwa katika Sekta rasmi wamebebeshwa mzigo mkubwa wa kulipa kodi. Aidha, posho na marupurupu ya mfanyakazi visitozwe kodi kwa kuwa tayari mfanyakazi huyo ameshabeba mzigo mkubwa na kipato chake ni kidogo.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa sasa haukubadilisha sheria ya zamani katika utozaji kodi ya mapato yatokanayo na ajira. Hivyo, mfanyakazi ataendelea kutozwa kodi yake kama alivyokuwa anatozwa hapo zamani. Aidha, ili kuondoa utata katika tasfiri ya sheria, mabadiliko katika rasimu ya kwanza ya Muswada yamefanyika na sasa Muswada utatumia maneno yale yale yanayotumika katika sheria ya sasa hasa kuhusiana na utozaji kodi katika posho wanazolipwa watumishi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo haya, mapato yafuatayo kwa mfanyakazi hayatatozwa kodi: -

(i) Huduma za chakula zinazotolewa na mwajiri katika sehemu ya kazi bila ya ubaguzi;

(ii) Gharama ya matibabu ya mfanyakazi pamoja na familia yake;

(iii) Nauli ya likizo kwa mfanyakazi na familia yake;

(iv) Posho ambazo zinafidia gharama zinazohusiana na ajira;

(v) Posho za kujikimu na zinazohusu huduma kwa Majimbo ya Uchaguzi;

(vi) Thamani ya nyumba itolewayo na mwajiri ambaye ni Serikali au Asasi ambayo mapato yake yanatokana na Bajeti ya Serikali;

(vii) Matumizi ya gari kwa wafanyakazi wa Serikali au Taasisi za Serikali; na

(viii) Kiinua mgongo cha Wafanyakazi wa Serikali na Asasi zake pamoja na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya kupanua wigo wa kodi kujumuisha uwezeshaji wa Wananchi na kurasimisha Sekta isiyo rasmi. Hoja hii inakubalika na ni sehemu ya mkakati wa Serikali wa kupanua wigo wa kodi kama ilivyoelezwa wakati wa kuwasilisha Muswada. Sababu kubwa ya kuwezesha Wananchi na kurasimisha sekta

isiyo rasmi siyo kuwatoza kodi, bali kuondoa umaskini na kukuza uchumi. Hatua kadhaa za kutekeleza sera ya uwezeshaji zitapendekezwa kwenye Bajeti ya mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, ilitolewa hoja kwamba, *excess liquidity* kwenye Mabenki kwamba, ielekezwe kwenye Sekta za uzalishaji mali hasa kilimo. Ni kweli kwamba, Mabenki yetu yana fedha nyingi za ziada ambazo hayajaweza kuzikopesha kwa wateja. Tatizo hili linatokana na mazingira magumu katika Sekta ya Fedha nchini, hasa ukosefu wa taarifa kuhusu wakopaji, uaminifu wa wakopaji, sheria zinazomlinda zaidi mkopaji kuliko mkopeshaji na kadhalika. Hatua zilizokwishachukuliwa ni pamoja na zifuatazo: -

(i) Kuhamasisha Mabenki kuanzisha *Credit Information Bureau* ili wateja wazuri wapate mikopo kwa urahisi;

(ii) Marekebisho ya kisheria ili kuweka uwiano mzuri wa ulinzi kwa mkopaji na mkopeshaji, kwa mfano, Sheria ya Ardhi;

(iii) Kuanzishwa kwa Mahakama ya Biashara ili kurahisisha pamoja na mambo mengine, mashauri kati ya Mabenki na wateja; na

(iv) Mifuko ya kudhamini mikopo katika Sekta muhimu, hii ni pamoja na *Export Credit Guarantee Fund* unaodhamini mikopo ya Vyama vya Ushirika kwa ajili ya mazao ya biashara, *SME Credit Guarantee Fund* na *Development Finance Guarantee Fund,* kwa ajili ya mikopo kwa miradi mikubwa katika Sekta za Kilimo na Viwanda.

Mheshimiwa Spika, ilitolewa pia hoja ya *tax holidays* kwamba, zinatumiwa kukwepa kodi. *Tax holidays* zilianza kutumika nchini kwa mujibu wa Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1990 *(The National Investment Promotion and Protection Act, 1990 - NIPPA).* Sheria hiyo ilitoa *holiday* ya miaka mitano kwa wawekezaji waliopata hati za *Investment Promotion Center (IPC).* Sheria ya *NIPA* ilifutwa na *Tanzania Investment Act* ya 1997, ambapo *tax holidays* ziliondolewa pia isipokuwa kwa wawekezaji waliokuwa tayari wamo ndani ya hizo *holidays. Holidays* zilikwisha mwaka 2002. Vivutio hutolewa kwa misingi ya uwekezaji uliofanywa, siyo jina la mwekezaji. Kwa hiyo, mabadiliko ya mmiliki wa mradi hakumpatii mmiliki mpya kivutio mpaka atakapokuwa amewekeza. Kwa hiyo, tahadhari ya kutosha imechukuliwa katika sheria ili pasiwe na udanganyifu.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Madini haina *tax holidays* isipokuwa gharama za mtaji *(Capital Expenditure)* hutolewa zote katika mwaka zinapolipwa *(100 percent expensing of capital expenditure).* Hii ni kwa kuzingatia gharama kubwa za kutafuta madini na kujenga mgodi. Baada ya gharama hizo kufidiwa, Makampuni haya yatalipa *corporation tax* kama walipakodi wengine. Aidha, Sekta hii inafanyiwa uchambuzi na Tume iliyoundwa na Serikali na masuala ya kodi yatajumuishwa katika uchambuzi huu.

Mheshimiwa Spika, ilitolewa hoja kwamba, mabadiliko haya ya Sheria ya Kodi ya Mapato yataongeza mapato kwa kiasi gani. Muswada umeandaliwa ili kuziba mianya ya kukwepa kodi, kupanua wigo na kuongeza *compliance* kwa kuifanya sheria kuwa rahisi zaidi kueleweka. Kila moja ya hatua hizi inategemewa kuongeza mapato lakini si rahisi kwa sasa kufahamu ni kwa kiasi gani. Ingawa tunafahamu kwamba, mianya iliyozibwa ilikuwa inatumiwa vibaya, lakini hatujui kwa uhakika kodi iliyokuwa inakwepwa ni kiasi gani, vivyo hivyo kwa maeneo yaliyobakia. Hivyo, tunajua marekebisho haya yatatuwezesha kukusanya mapato mengi zaidi , lakini hatujui hiyo ziada ni kwa kiasi gani, tunaomba tuvute subira tuone matokeo ya sheria hii.

Ilitolewa hoja kuhusu elimu na huduma kwa walipakodi iboreshwe ili kumfanya mlipakodi alipe kodi kwa hiari na kwa urahisi. Mojawapo ya malengo makuu ya Muswada huu ni kurahisisha uelewa na matumizi ya sheria yenyewe. Ili kupata hili yafuatayo yamefanyika: -

(i) Kuwianisha kanuni za ukadiriaji wa mapato yanayotozwa kodi na zile zinazotumika kukokotoa faida au mapato katika hali ya kawaida. Kwa hiyo, mtu yeyote mwenye ujuzi wa biashara na uhasibu atakuwa Mtaalam wa Kodi pia;

(ii) Uanzishwaji wa utaratibu wa mlipakodi kujikadiria mwenyewe ambao utaondoa na kupunguza usumbufu na mazingira ya rushwa katika ukadiriaji;

(iii) Muswada katika kifungu cha 108(1) unabainisha hatua za kuchukua endapo mfanyakazi katika Mamlaka ya Mapato atakiuka taratibu na kwenda kinyume cha sheria;

(iv) Kuweka wazi kanuni na taratibu za utekelezaji wa Muswada *(Practice Notes).* Kanuni hizi zitagawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge; na

(v) Aidha, mamlaka ya mapato itaendelea kutoa elimu kwa walipakodi kupitia machapisho, semina, mikutano, magazeti pamoja na vipindi vya redio na televisheni.

Mheshimiwa Spika, ilitolewa hoja kwamba, kiwango cha chini cha mapato ya watu binafsi yanayotozwa kodi kiongezwe. Viwango vya kodi vilivyoainishwa katika Ibara ya kwanza ya jedweli la kwanza la Muswada ukurasa wa 129, inawahusu watu binafsi ikijumuisha waajiriwa na waliojiajiri wanaoandaa hesabu kamili za biashara zao. Katika kupanga viwango hivi ni muhimu kuzingatia hali halisi ya mapato ya makundi husika na umuhimu wa kila raia kuchangia katika gharama za huduma za msingi za jamii. Pamoja na kupanua kima cha chini cha mshahara, uwezo wa Serikali wa kuwalipa watumishi wake umeendelea kuwa kigezo cha kupima kiwango cha mapato ambapo mhusika anatakiwa kutoa mchango kwa njia ya kodi. Kwa kawaida kima cha chini cha mshahara Serikalini, ni juu ya kima cha chini kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, Serikali inachukua hoja hii ya Waheshimiwa Wabunge, ili iifanyie kazi na kuleta majibu katika bajeti ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ilitolewa hoja kwamba, Muswada huu ungetanguliwa na Tume kabla ya kuandaliwa na kuletwa Bungeni. Tume huundwa ili kuandaa sera siyo kuandika sheria. Katika mifano yote iliyotolewa na mtoa hoja, Serikali ilikuwa inatafuta kuandaa sera muafaka kujibu hoja zilizokuwa zimejitokeza. Utaratibu wa kutumia Tume hutumia muda mwingi sana na kwa gharama kubwa. Kimsingi sera za kodi za sasa zina misingi yake katika Ripoti ya Tume ya Mtei ya mwaka 1989.

Mheshimiwa Spika, ilitolewa hoja kwamba, hakuna uwiano katika viwango vya kodi kwa mapato kutokana na ajira na kutokana na biashara katika ibara ya kwanza na ya pili za jedweli la kwanza la Muswada. Katika jedwali linalohusu wafanyabiashara wadogo wadogo, *presumptive tax* katika jedweli la kwanza ibara ya pili tunatumia mauzo *(turn-over)* siyo faida au *net income*. Katika ibara ya kwanza viwango vya mapato yaliyotajwa ni mapato halisi baada ya kutoa gharama za ajira, biashara na uwekezaji. Kwa hiyo, siyo sahihi kulinganisha viwango hivi.

Mheshimiwa Spika, ilitolewa hoja kwamba, Halmashauri zisitozwe kodi zaidi ya viwango vilivyowekwa katika Muswada huu. Kwa mujibu wa sheria zetu na mgawanyo wa madaraka baina Serikali na Serikali za Mitaa, Serikali za Mitaa zina madaraka ya kutoza kodi fulani, lakini siyo kodi zile zinazotozwa na Serikali Kuu. Baada ya maamuzi ya mwaka 2003, kodi ambazo Halmashauri zinaweza kutoza sasa ni bayana.

Mheshimiwa Spika, ilitolewa hoja kwamba, sekta isiyo rasmi ijumuishwe katika wigo wa kodi. Ningependa tu kusema kwamba, hatua za kupanua wigo zilizoelezwa katika maelezo ya kuwasilisha Muswada zinahusu pia sekta binafsi kwa mfano, urahisishaji wa sheria, *practice notice, presumptive tax* na kadhalika.

Pia hatua ya kwanza ya kujumuisha sekta isiyo rasmi katika wigo wa kodi ni kuiingiza sekta yenyewe katika uchumi rasmi. Hivyo, hatua za kurahisisha kurasimisha sekta hii zilizokwishaanza zinajibu hoja hii.

Mheshimiwa Spika, pia ilitolewa hoja kwamba, sheria ya uwezeshaji iletwe Bungeni. Jibu kwa hoja hii ni kwamba, Serikali imeshaanzisha sera na sheria itakuja kwa wakati wake.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ilitolewa hoja kwamba, je, sadaka katika Taasisi za Dini, zitapata unafuu chini ya kifungu cha 16? Jibu ni hapana, sadaka hazitapatiwa unafuu. Lakini taasisi hizo zitaendelea kupata msamaha chini ya kifungu cha 64. Vifungu husika vinarekebishwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea naomba nikiri kufarijishwa sana na michango iliyotolewa na Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi na Mwakilishi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Grace Kiwelu na Wabunge. Mawazo yenu kama kawaida tumeyachukua na kwa kweli

hasa yale ya Kamati ya Fedha na Uchumi, tulikwisha yachukua na kuyafanyia kazi katika mabadiliko ambayo tayari tulikwisha wasilisha pamoja na Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa nifafanue kidogo kwamba, wasiwasi wa Mheshimiwa Grace Kiwelu, tulikwisha ujibu, Mheshimiwa Grace Kiwelu alikuwa na wasiwasi juu ya kodi kwa wafanyakazi. Lakini kama nilivyokwishaeleza, ule wasiwasi haupo tena kwa sababu tumekuja kuziondoa na kuacha hali ilivyokuwa *(status quo),* hatukufanya jambo lolote ambalo halikuwa linafanywa huko nyuma na hata maneno yaliyokuwa yanatumika huko nyuma yale ya mwaka 1973 tumeyarejesha.

Kwa hiyo, kusiwe na wasiwasi juu ya wafanyakazi na ningependa kusisitiza hasa kwa wafanyakazi waelewe vizuri kwamba, mapato yafuatayo hayatatozwa kodi ya wafanyakazi:-

(i) Huduma ya chakula *(Cafeteria Services),* wale ambao wanapata huduma za chakula kwenye *canteen* za viwanda vyao;

(ii) Pili gharama za matibabu za wafanyakazi na familia zao zinazofanywa na mashirika yao;

(iii) Nauli ya likizo kwa mfanyakazi ile nauli haitapigwa kodi kama tulivyokuwa tumependekeza mwanzo, kwao na familia zao; *(Makofi)*

(iv) Posho ambazo zinafidia gharama zinazohusiana na ajira hizo hazitapigwa kodi; *(Makofi)*

(v) Posho za kujikimu na zinazohusu huduma, hata zile zinazohusu huduma kwa Majimbo ya Uchaguzi kwa ajili ya Wabunge *(Jimbo allowance)* zile hazina kodi; *(Makofi)*

(vi) Thamani ya nyumba itolewayo na mwajiri ambaye ni Serikali au Asasi ambayo mapato yake yanatokana na Bajeti ya Serikali hiyo hamna kodi; *(Makofi)*

(vii) Matumizi ya gari kwa wafanyakazi wa Serikali au Taasisi ya Serikali hamna kodi; na *(Makofi)*

(viii) Mwisho, kiinua mgongo cha wafanyakazi wa Serikali na hata pia cha Wabunge hakuna kodi, kwa hiyo, kwa kweli haya tulishaleta kwenye marekebisho ambayo tumefanya. Tumaini langu ni kwamba, wafanyakazi wanaweza sasa wakafanya kazi na kuongeza tija, kwa sababu la msingi ni waweze kujiongezea mshahara kwa hiyo wasiwasi hautakiwi kuwepo tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili la kupanua wigo na kuangalia hali za watu wadogo, wafanyakazi wa kawaida na watu wasio katika sekta rasmi, kwanza mimi nafurahi sana kwamba, Waheshimiwa Wabunge, wameona umuhimu wa kuingiza kila mtu kwenye wigo wa kodi, kila mtu hata kama ni mdogo aingie kwenye wigo wa kodi. Pamoja na ahadi tuliyotoa kwamba, tutaangalia tena upya, ni kiwango gani. Sasa hivi kima cha chini kwa mfanyakazi wa kawaida kilicho kwenye sheria ni shilingi 48,000/=, kima cha chini

kwa mfanyakazi Serikalini, katika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ni shilingi 55,000/=. Licha ya marupurupu haya mengine yote huku ambayo nimesema hatutayatoza kodi.

Kwa hiyo, kama hoja sasa ni kwamba, hata hao wasilipe kodi hawa wa vima vya chini viwili hivyo, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, tuko tayari kuangalia tena upya. Lakini ningetaka kutoa *caution* kwamba, kodi inayotokana na wafanyakazi ni sehemu muhimu sana ya mapato ya Serikali kwa sababu wafanyakazi ni eneo kubwa. Kwa bahati nzuri *actually* ndiyo yenye uhakika. Mimi nikiwa na wafanyakazi 200 nina uhakika nitakusanya kodi kwa wafanyakazi 200. Lakini nikiwa na Machinga 200 sina uhakika au Mama Ntilie 200, sina uhakika kama nitakusanya kodi kwao. Hawa ni watu wa uhakika na ndiyo maana kwenye jedweli la kwanza nafikiri ni ukurasa wa 130 wa Muswada, tumeweka namna tunavyotaka kutoza hawa wadogo kodi na kama utakavyoona tumejaribu sana kutowatoza kodi kubwa. Nafikiri kwa *informal sector* hawa ni kati ya shilingi moja na shilingi milioni tatu tumeweka shilingi 20,000/=. Wewe unapata kwa mwaka shilingi milioni tatu tunakutoza shilingi 20,000/=. Nakubali kwamba, mfanyakazi ambaye anapata shilingi milioni tatu analipa zaidi kuliko huyo mtu aliye kwenye sekta isiyo rasmi anayelipa shilingi 20,000/=. Lakini lazima tuanze mahali kwa sababu huyu mtu wa shilingi 20,000/= naye ana gharama nyingi ambazo hazifidiwi, akienda hospitali anajilipia, kila mahali anajilipia na anajitegemea. Kwa hiyo, lazima tuangalie pia namna ya kumsaidia huyu mtu kwa sababu yeye, nia kubwa ni kumwezesha ili aweze kuongeza mapato yake ya biashara na aweze kukua. Hata hivyo, kama nilivyosema tutaangalia jambo hili nitalipeleka kwenye Kamati ya Kodi ndani ya Wizara ya Fedha, ili tuone namna ya kulishughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili la *excess liquidity* niongee tu katika mabenki, hili ni tatizo kubwa. Nusu ya fedha zilizoko kwenye benki zimelala huko, nusu ile haizunguki. Kwa hiyo, tumeanza mazungumzo na wenye mabenki kuona namna ya kutumia hizo fedha ambazo zimezubaa.

Lakini labda tunaweza tukazitumia kwa namna moja ya kuelewana nao kusaidia sekta kama za kilimo, sekta kama ya viwanda na shughuli ndogo ndogo haya ni mambo tunazungumza nao ili baadaye tuweze kuona kwamba jambo hili haliendelezwi tena. Lakini la msingi sana ni mabadiliko yaliyofanywa katika sheria. Uzoefu tulionao sasa hivi baada ya kuchukua hatua mbalimbali, kwa mfano, ile Sheria ya Ardhi, kuwa na hii mipango ya kudhamini wakopaji na sasa hivi kuna mpango mwingine wa kujua wasiorudisha madeni ni kina nani. Labda haya yote yatasaidia kuzifanya benki ziweze kukopesha vizuri zaidi.

Sekta ya Madini ilizungumziwa niseme tu kwa kifupi kwamba, Sekta ya Madini ni kubwa na nyeti na imeundiwa Kamati Maalum na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kamati Maalum inachunguza ili iweze kushauri Serikali hatma ya masuala ya kodi kwenye sekta hii. Kwa hiyo, jambo hilo litakapokamilika, tutakuja hapa tena na mapendekezo mapya ya namna sekta hii inavyoweza ikachangia kwenye masuala ya kodi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na mazungumzo mengi juu ya sasa hawa wakadiriaji wa Mamlaka ya Mapato wawe na huruma, wawe waelewa. Ukweli sheria hii imeweka masharti fulani ya namna mkadiriaji atakavyohusiana na anayedaiwa kodi.

Lakini la pili tumechukua hatua nyingine za kiutawala. Kuanzia miezi 9 iliyopita ndani ya Mamlaka ya Kodi, mtumishi asiyefuata maadili yake ya kazi atashughulikiwa na Kamati za Maadili. Kwenye shirika hili tumeunda Kamati za Maadili na zimefanya kazi kwa miezi 9. Kwa miezi 9 hiyo wafanyakazi 45 wamekwishaitwa kwenye Kamati hizo za Maadili. Kati ya hawa 45, wafanyakazi 9 wamekwishapelekwa kwenye Tume ya Kuzuia Rushwa *(PCB),* wakachunguzwe zaidi na vyombo hivyo ili kama ni wanahusika waweze kushughulikiwa kisheria. Kwa hiyo, jambo hilo sisi hatuna wasiwasi na limeleta nidhamu sana, Kamati hizi ziko ngazi ya Wilaya, Mkoa mpaka Makao Makuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo kwa kawaida Waheshimiwa Wabunge, wasingelifahamu ni kwamba, toka shirika hili lianzishwe wafanyakazi 248 wamekwishafukuzwa. Maana tumeulizwa wamechukuliwa hatua gani? Walikwishafukuzwa kwa makosa yanayohusiana na maadili na hisia za rushwa na unyanyasaji wa walipa kodi na kadhalika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sasa hivi kwa kweli sisi tunaona kuna mabadiliko makubwa. Hivi karibuni kama sehemu ya mpango wa miaka 5 wa maendeleo ya Mamlaka ya Mapato, tumeanzisha kitu kinachoitwa mtoza ushuru kamili *(Total Tax Person),* maana yake ni kwamba, huko nyuma mamlaka ilikuwa na mgawanyiko. Kuna mtu anayeitwa huyu ni wa forodha, huyu anaitwa ni wa *revenue*, huyu anaitwa ni wa *VAT* na kadhalika, mpaka huko Wilayani. Kwa hiyo, unaweza kwenda kwenye Wilaya au Mkoa ukakuta hizo ofisi zimetawanyika ziko kila mahali, unatoka hapa kwenda pale. Sasa hivi kuna mtu mmoja tu ambaye ni *boss*, utaratibu wa sasa kila mtumishi wa mamlaka atafahamu kazi ya kila shughuli ya mamlaka ndiyo *total tax person.*

Kwa hiyo, kwa kutegemea tu mahali na wakati wewe unaweza ukafanya kazi za *VAT,* mwingine akafanya kazi fulani, lakini vile vile unaweza ukatoka kwenye *VAT* ukahamishwa kwa *custom*, ukatolewa kwenye *custom* ukahamishwa kwenye kodi ya mapato na kadhalika. *(Makofi)*

Wakati tunafanya jambo hilo tumewapeleka wote shule, wafanyakazi wakubwa wote wa Wilaya na Mkoa na Taifa wamerudishwa shuleni. Tuna Chuo cha Kodi pale Dar es Salaam na Wajumbe wa Kamati ya Fedha ni mashahidi, wao walipelekwa kwenye chuo kile kwa siku tano, wakijifunza Muswada huu. Sasa hivi hapa tuna watalaam, Kamati ya Fedha na Uchumi kwa kweli wamekuwa watalaam, wamekwenda darasani mimi ninawapongeza, siyo rahisi kwa Mbunge kukaa darasani. Hawa walipelekwa darasani kwa siku tano kwa kuomba wao wenyewe. Maana unajua kuna ile Kanuni ya Chama cha Mapinduzi, inayosema: “nitajisomesha mpaka mwisho wa maisha yangu”. Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Fedha na Uchumi, wametii na kurudi darasani kujisomesha mpaka walipoelewa sawa sawa hii sheria ndiyo maana hapa tatizo halikuwa kubwa kwa sababu uelewa ulikuwa mkubwa, lakini waliketi darasani kwenye chuo kile wakasoma sheria hii. Kwa hiyo, wanaielewa sasa kwa kiasi kikubwa, hawawezi kuwa *tax expert* kwa sababu watu wanapata *Ph.D.* kwenye mambo ya kodi, lakini angalau wapate mwanga, wasiwe mbumbumbu zaidi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wakubwa wao wa Shirika hili walipelekwa shuleni hapo, baada ya zoezi hilo ngazi ya Wilaya wakapewa mtihani, walioshinda mtihani waliteuliwa wakawa Wakuu wa Wilaya wa Mamlaka ya Mapato, wale walioshindwa walipewa nafasi ya pili, walioshindwa tena waliteremshwa cheo na wengine waliambiwa *bye bye* kwa sababu unafanya nini wewe dreva kama hujui hata jinsi ya kubadilisha *gear* utaendeshaje gari? Hivi mwezi uliopita ndiyo wale Wakuu wa Mkoa walikuwa nao wanapigwa msasa kule Dar es Salaam. Wamerudi huko kumetokea mabadiliko, wengine wamehamishwa wengine wamerudi kwenye vituo vyao. Utaratibu utakuwa hivyo utapewa mtihani wa kile unachofanya unakielewa? Anayeshinda atabaki, anayeshindwa anapewa nafasi moja, akishindwa tena *bye bye.* Tunataka shirika hili liwe *professional.* Kazi ya kodi siyo kazi ya kubahatisha, unakurupuka tu unafanya! Ndiyo wengine walikuwa kwa kweli wanatumia marungu ni kwa kutojua kwa sababu unajua mlipa kodi akikuuliza swali la kitalaam huwezi kumjibu kwa hiyo, unamlazimisha kwa sababu huna sheria, *no* lazima umuelimishe *you have to be persuasive.* Lazima umuelimishe aelewe na akubali, yaani utumie nguvu ya hoja siyo hoja ya nguvu tu. Kwa hiyo, tumaini langu ni kwamba, tunafanikiwa. *(Makofi)*

Jambo la tatu ambalo limefanyika, Makao Makuu kila mwezi wanafanya mikutano na wadau wakubwa kuwasikiliza, ehee! Mnasemaje sasa? Mna malalamiko gani na kadhalika. Mikutano ambayo wamekwishafanya mpaka sasa hivi iko kama mitatu hivi. *Feedback* niliyoipata mimi walipa kodi wamefurahi sana wamesema kumbe hawa watu walikuwa na utu kiasi hiki walikuwa wapi? Maana yake wameelimishana kumbe kuna mtu analalamika pale kumbe tatizo lake haelewi. Sasa wanaelimishana. Kuna mtoza ushuru ambaye naye alikuwa anakoroma tu kwa sababu haelewi wanaelimishwa. *Both ways* nchi inafaidika na watu wanalipa kodi kwa hiari. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hili ni shirika jipya unaweza ukasema hivyo. Kwa nini tunaweza tukasema shirika jipya? Kwa sababu mimi nilifika mahali nikaona shirika hili limefanya kazi nzuri lakini tumefika katikati ya njia, lazima tufanye kitu kinachoitwa *midterm review.* Tukafanya *midterm review* tukapanga safu upya sasa shirika linakwenda kitaalam, kitalaam maana yake ni kisheria na kufuata kanuni na maadili ya watoza ushuru popote walipo. Kwa hiyo, mimi sina wasiwasi kabisa kwamba, kwa njia hii uhusiano kati ya watumishi wa mamlaka na walipa kodi utakuwa mzuri na mlipa kodi akishakuwa na imani na mtoza ushuru atalipa kwa hiari, kitu kinachoitwa *compliance* atalipa kwa hiari na tayari tumekwishaona na ndiyo maana sisi hatuna wasiwasi juu ya dhana ya *self assessment.*

Tunamwambia wewe si ulikuwa unalalamika kwamba, unaburuzwa na wale watu wa kodi, sasa tuambie wewe unataka kulipa kiasi gani, analipa, sisi tuna namna ya kumfuatilia yule bwana, tunafanya kitu kinachoitwa *exception,* tunakagua *by exception,* leo tunasema tutakwenda kwa huyu na yule na yule kwa makundi. Halafu kati ya walipa kodi kuna kundi lenye panono na kundi ambalo halina panono. Sisi hatuwezi kukimbilia mifupa, tena mifupa ya mbuzi, tutakimbilia panono. Wamasai wanaelewa hiyo lugha. Unapokula nyama ukila mfupa wa mbuzi ni tofauti kabisa na mfupa wa ng'ombe dume. Sisi wa Kilimanjaro tunaelewa kidari. Sisi lazima twende kwenye kidari ndipo kwenyewe kwa mzee! Pale ndiyo tunapotaka tupate mafuta sawa sawa pale. Kwa hiyo, hata hiyo *self*

*assessment* hatutawafuata ambao tunajua wao ni *peripheral, marginal,* tutafuata pale pazuri kwa mfano eneo la mafuta *(fuel)* tutafuata watu wanaouza mafuta. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, juzi juzi utakumbuka kwenye bajeti hii tuliyonayo sasa, Waheshimiwa Wabunge, walikubali hatua ambazo nilipendekeza zichukuliwe kwenye eneo la mafuta. Nataka kutoa taarifa kwamba, toka wakati ule kodi inayotokana na mafuta imeongezeka kwa shilingi bilioni 5 kila mwezi. Kama walikuwa wanatoa shilingi bilioni 12 sasa zimekuwa shilingi bilioni 17, bilioni 18 na bado hatua ya mwisho katika mtiririko ule sijaichukua, Mwezi wa 7 inachukuliwa hatua ya kufunga mita. Nadhani alikuwa Mheshimiwa Yete Mwalyego, alikuwa analalamika hapa jana, ikifika Mwezi wa 7 nitafunga mita fulani ili pale mafuta yanapoingia hivi ile mita inaonyesha tu kiasi inasoma, inaona ni kiasi gani. Bado nitapata fedha zaidi kwenye mafuta. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wale wanaouliza nyie mmekadiria mapato mapya ni nini? Hapana, tuna uzoefu. Unajua kukadiria ni takwimu unaweza ukaketi ofisini ukakadiria ni takwimu. Sisi tuna uzoefu, tunajua ukigonga kwenye mafuta utapata, ukigonga kwenye almasi utapata, ukigonga kwenye dhahabu utapata, uzoefu tunaotaka kuutumia zaidi kuliko hata nadharia za kitakwimu. Ndiyo maana tuna uhakika kwamba, sheria hii itaongeza mapato kabisa, itaongeza mapato, yapo. Kwenye mtungi wowote lazima ujue kijiko cha namna utakavyoingiza ili uweze kupata sawa sawa. Hii ndiyo yenyewe sisi tulikuwa na uhondo mkubwa kwenye chungu, lakini tulikuwa hatuna namna ya kuchota ili tupate sawa sawa ndani ya chungu kile. Sheria hii itatufikisha hapo.

Mimi nina uhakika na naamini kabisa kwa sababu ya uzoefu kuliko hata takwimu za kinadharia. Ndiyo maana ile hoja nadhani alikuwa Mheshimiwa Nimrod Mkono ya kwamba tuunde Tume. Ya kutuaambia nini zaidi, kwa sababu tunaona hizi fedha, tunaziona. Tume ya kutuambia nini zaidi, kwanza tuteke haya tunayoyaona. Maana hizi Tume ni gharama kubwa ya pili zinachukua muda mrefu. *(Makofi/Kicheko)*

Mimi nataka nimalize hii kazi kabla ya 2005, sasa ukiunda Tume leo itaripoti mwaka 2010, mimi ninataka hela kwenye bajeti ijayo, nisipoipata kwenye bajeti ijayo nitaongeza kodi mahali pasipofaa, lazima niongeze kodi mahali pasipofaa, maana yake Serikali lazima ifanye kazi. Mimi sitaki kuongeza kodi mahali pasipofaa nataka kuchota kile ninachoona. Kwa hiyo, mimi nashukuru mmenielewa hivyo na tutafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nifafanue vizuri hili jambo la sadaka. Nadhani Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, alisemea sadaka na mapato. Niseme wazi kwamba, kwa bahati mbaya hata madhehebu yetu yanaendeshwa na binadamu. Kwa sababu hiyo kuna siku nyingine nao wanafanya madudu yao. Hao wenye madhehebu sisi tumesema tutasamehe madhehebu kwa utaratibu uliko kwenye sheria hii. Lakini madhehebu nayo wanajua hatutaki kuyasemasema maana siyo heshima kwa Madhehebu na Mungu labda anaweza asituelewe tunawasema watu wake hapa. *(Kicheko)*

Lakini kweli wana madudu, *tax evasion, tax avoidance* ziko kwenye madhehebu kama zilivyo uraiani ni kweli. Sasa wewe ukienda ukaanzisha *tour company* ukaiita *St. Joseph* na watu wote waamini kuwa ni shughuli ya Kanisa la Kikristo, shughuli ya Mungu, ukaenda tena huko ukaanzisha *import export company* ukaiita ya Msikiti fulani. Sisi lazima tupate ushahidi sawa sawa ili tuweze kusamehe kodi inayotokana na shughuli ile.

Sisi tunasema ukienda kuanzisha *tour company* ukaiita *St. Joseph* italipa kodi mpaka utuonyesha faida inayotokana na *St. Joseph Tours* imetumikaje kuendeleza madhumuni ya Kanisa la *St. Joseph* au Msikiti wa Kwa Mramba. Biashara hii inaitwa *export import* na wenye mali ni Msikiti wa Kwa Mramba. Sasa twende kule kwa Msikiti wa Kwa Mramba, tuone hii hela inatumikaje ndani ya Msikiti wa Kwa Mramba au kwa madhumuni ya Msikiti ule wa Mramba la sivyo lazima ulipe kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata wa madhehebu ya dini wajue kwamba, tumesamehe, lakini kwa kweli lazima na wenyewe wafanye mambo yaliyo *neat* au *clean*. Nimalizie kwa kusema sheria hii siyo ya chuma cha pua *(is not steel),* tutaendelea kuwa *flexible* katika utekelezaji. Nikiona jambo haliendi vizuri narudi hapa, *Financial Bill* inamalizia. Tunaelewana hapa hapa tunarekebisha. Lazima iwe *flexible* sana.

Mwisho kabisa, Mheshimiwa mmoja, nadhani alikuwa Mheshimiwa Semindu Pawa, alikuwa anasemea siku kuu ya walipa kodi. Hakuna nchi yenye siku ya walipa kodi. Iko Rwanda, Rwanda ina siku kuu ya walipa kodi. Mwezi uliopita walikuwa na hiyo siku kuu. Walitualika sisi, Shirika langu lilikwenda. Wanapewa zawadi waliolipa kodi vizuri. Rais ana zawadi zake, Spika ana zawadi zake, Jaji Mkuu ana zawadi zake, Waziri wa Fedha ana zawadi zake. Ni sherehe inayofanywa toka asubuhi mpaka jioni. Toka mawio mpaka machweo. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, kule Rwanda wameanza na hata sisi tunawaangalia kwa uangalifu vile vile. Labda siku moja tutoe hata vyeti, hata tuwatambue tu walipa kodi. Kwa hiyo, Rwanda kuna *Tax Day, Tax Payers Day* iko hiyo siku. *(Makofi)*

Ningependa niwashukuru kwa jinsi mlivyonielewa. Tulianza mbali. Huko mitaani kwanza maneno mengi mengi yamesemwa. Lakini tumemalizia pazuri. Naomba mnipe, kwa sababu hii kama nilivyosema hiki ndicho kijiko cha kunisaidia kuchota vizuri kwenye kile chungu ili hapa mniulize mbona hiki hakiendi vizuri, mbona hiki hakileti matokeo. Lakini nawaahidi kitaleta matokeo.

Mheshimiwa Spika, naomba tena kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Kodi ya Mapato wa Mwaka 2004**
***(The Income Tax Bill, 2004)***

**SPIKA:** Shughuli za Kamati zimeanza. Kama mnavyoona Waheshimiwa Wanakamati wa Bunge Zima, Muswada ni mrefu sana, una vifungu vingi, viko vifungu 145, kwa hiyo, tutatumia ule utaratibu wetu wa kawaida wa sehemu kwa sehemu badala ya kifungu kwa kifungu. Tunaendelea Katibu.

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 3
Kifungu cha 4
Kifungu cha 5

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu cha 6

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 7
Kifungu cha 8
Kifungu cha 9

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu cha 10

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 11

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu cha 12
Kifungu cha 13

Kifungu cha 14

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu cha 18

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 19
Kifungu cha 20
Kifungu cha 21
Kifungu cha 22

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 27

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu cha 28
Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31
Kifungu cha 32
Kifungu cha 33
Kifungu cha 34
Kifungu cha 35

Kifungu cha 36
Kifungu cha 37

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 38
Kifungu cha 39

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu cha 40
Kifungu cha 41
Kifungu cha 42
Kifungu cha 43
Kifungu cha 44
Kifungu cha 45
Kifungu cha 46
Kifungu cha 47
Kifungu cha 48
Kifungu cha 49
Kifungu cha 50
Kifungu cha 51
Kifungu cha 52
Kifungu cha 53
Kifungu cha 54
Kifungu cha 55
Kifungu cha 56
Kifungu cha 57
Kifungu cha 58

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 59

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu cha 60
Kifungu cha 61
Kifungu cha 62
Kifungu cha 63

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 64

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu cha 65
Kifungu cha 66
Kifungu cha 67
Kifungu cha 68
Kifungu cha 69
Kifungu cha 70

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 71
Kifungu cha 72
Kifungu cha 73
Kifungu cha 74
Kifungu cha 75
Kifungu cha 76
Kifungu cha 77
Kifungu cha 78
Kifungu cha 79
Kifungu cha 80

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu cha 81

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 82
Kifungu cha 83
Kifungu cha 84

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu cha 85
Kifungu cha 86
Kifungu cha 87

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 88
Kifungu cha 89

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu cha 90

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 91

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu cha 92
Kifungu cha 93

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 94

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu cha 95
Kifungu cha 96
Kifungu cha 97

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 98
Kifungu cha 99
Kifungu cha 100

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu cha 101
Kifungu cha 102
Kifungu cha 103

Kifungu cha 104
Kifungu cha 105
Kifungu cha 106

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 107
Kifungu cha 108
Kifungu cha 109

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu cha 110
Kifungu cha 111

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 112
Kifungu cha 113
Kifungu cha 114

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu cha 115
Kifungu cha 116

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 117

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu cha 118
Kifungu cha 119
Kifungu cha 120
Kifungu cha 121
Kifungu cha 122
Kifungu cha 123
Kifungu cha 124
Kifungu cha 125

Kifungu cha 126
Kifungu cha 127
Kifungu cha 128
Kifungu cha 129
Kifungu cha 130
Kifungu cha 131
Kifungu cha 132
Kifungu cha 133
Kifungu cha 134
Kifungu cha 135
Kifungu cha 136
Kifungu cha 137
Kifungu cha 138
Kifungu cha 139
Kifungu cha 140
Kifungu cha 141
Kifungu cha 142
Kifungu cha 143
Kifungu cha 144
Kifungu cha 145

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 1
Jedwali la 2
Jedwali la 3
Jedwali la 4
Jedwali la 5

*(Majedwali yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kodi ya Mapato wa Mwaka 2004**
***(The Income Tax Bill, 2004)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 *(The Income Tax Bill, 2004),* mafungu kwa mafungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Kwa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba Muswada huu sasa ukubaliwe rasmi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hatua za kuchukuliwa na Bunge zimekamilika juu ya Muswada huu. Sasa utakwenda kwa Mheshimiwa Rais, kupata kibali chake.

Kama nilivyokwisha kueleza, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 05.40 asubuhi Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**ND. KIPENKA M. MUSSA - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizokuwa zimepangwa kwa ajili ya Mkutano huu wa Kumi na Tano, sasa zimemalizika.

**SPIKA:** Kwa taarifa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Waziri Mkuu, atoe hoja ya kufunga Mkutano wa Bunge. *(Makofi)*

## KUAHIRISHA BUNGE

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kazi zilizokuwa zimepangwa zitekelezwe na Waheshimiwa Wabunge katika Mkutano huu wa Kumi na Tano, zimekamilika. Katika mkutano huu, jumla ya maswali 129 ya Waheshimiwa Wabunge yalijibiwa na Serikali. Majibu ya maswali hayo yameiwezesha Serikali kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali ambayo Waheshimiwa Wabunge waliyaulizia.

Kwa kutumia majibu hayo vile vile Serikali imeweza kuwafahamisha wananchi kazi mbalimbali zilizotekelezwa na Serikali na hatua zinazochukuliwa katika kuondoa kero kwa wananchi na vile vile kusaidia nguvu zao katika mapambano yetu dhidi ya umaskini. Katika mkutano huu vile vile Bunge lako Tukufu limepitisha jumla ya Miswada sita na kupokea taarifa za Kamati za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge kumpongeza Mheshimiwa Getrude Ibengwe Mongella, Mbunge wa Ukerewe kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Kwanza wa Bunge la Afrika. Sote tunatambua na kuthamini uwezo na uzoefu wake katika uongozi na hivyo hatuna shaka kuwa ataweza kukiongoza chombo hicho vema ili kiweze kukidhi matarajio ya Waafrika wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Umoja wa Afrika ni chombo kipya na Bunge la Afrika ni chombo kipya zaidi. Waafrika tuna matumaini makubwa na umoja huo na Bunge lake kuwa sasa na nguvu kubwa itaelekezwa katika kutatua migogoro isiyoisha Barani Afrika na kupambana na umaskini na maendeleo duni katika Bara letu. Tunakutakia Mheshimiwa Mongella na Bunge la Afrika unaloliongoza kazi njema. *(Makofi)*

Napenda vile vile kumpongeza Mheshimiwa Arcado Dennis Ntagazwa, Mbunge wa Kibondo na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia masuala ya mazingira, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Baraza la Mazingira Duniani. Tuna matumaini kuwa heshima hiyo aliyopewa siyo yake binafsi bali ni ya Taifa letu lote na kwamba chini ya uongozi wake Baraza hilo litaweza kusaidia jumuiya ya Kimataifa kupambana kwa nguvu zaidi na masuala ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira. *(Makofi)*

Aidha, nampongeza Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, Mbunge wa Maswa kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Baraza la Mawaziri wa Elimu Barani Afrika. Katika kipindi hiki ambacho Bara letu linatoa msukumo katika elimu kwa wote, ni heshima kubwa kwa nchi yetu kupewa jukumu la kuongoza chombo kinachowakutanisha viongozi wakuu wa elimu katika Bara letu. Ni matumaini yangu kuwa Mheshimiwa Dr. Ng'wandu atatumia ujuzi na uzoefu wake mkubwa katika sekta ya elimu kutoa uongozi utakaolisaidia Baraza hilo kuendeleza elimu ili tuweze kufikia malengo yote ya elimu kwa wote yaliyowekwa na Umoja wa Mataifa katika malengo ya Maendeleo ya *Millennium (Millennium Development Goals).*

Mheshimiwa Spika, wakati mkutano huu ukiendelea, tulipata taarifa ya kutokea ajali mbaya ya gari Wilayani Misungwi Mkoani Mwanza ambapo gari la abiria lilisombwa na maji na kutumbukia katika Mto Mwame. Hadi leo taarifa zinaonesha kuwa ajali hiyo imesababisha vifo vya watu 35. Kwa niaba ya Serikali, napenda kutoa salaam za rambirambi kwa ndugu na jamaa wa wale wote waliopoteza maisha na kutoa pole kwa wote walionusurika katika ajali hiyo. Kulingana na maelezo ya awali, ajali hiyo imesababishwa na uzembe wa dereva na ushawishi mbaya wa baadhi ya abiria. Ajali hii pamoja na nyingine ambazo zimetokea katika barabara zetu zingeliweza kuepukwa na kuokoa maisha ya watu wetu na uharibifu wa mali. Sote yaani Serikali, wenye vyombo na waendeshaji wao, watumiaji (wasafiri) na raia wengine wote tuna wajibu wa kupambana na matukio ya ajali hizi.

Kwa mfano, wanaosafiri kwa magari ya abiria mara kwa mara wanasita kuwakemea madreva ambao wanahatarisha maisha yao. Hata pale dreva anapoendesha kwa mwendo wa kasi unaohatarisha maisha, abiria ama hukaa kimya au wakati mwingine hata humshangilia jambo ambalo huwapandisha mori madreva na kuongeza mwendo zaidi. Napenda kutoa wito kwa Watanzania kuwa tuthamini maisha yetu na ya wenzetu na tuchukue hatua za tahadhari kila mara. Ingawa Waswahili husema: "Ajali haina kinga", ukweli ni kuwa ajali nyingi tungeweza kuzikinga au kuziepuka kama tungekuwa waangalifu, hasa wale wanaoendesha vyombo vya usafiri na watumiaji wengine wa barabara.

Mheshimiwa Spika, ajali nyingine ni za moto. Moto pia umekuwa ukileta hasara kubwa kwa kupoteza maisha na mali hasa katika miji yetu mingi. Ni vema Watanzania tukachukua tahadhari kubwa na kuhakikisha kuwa vifaa vya tahadhari ya moto na vya kuzimia moto vinakuwepo katika nyumba zetu na vinafanya kazi. Uangalifu uchukuliwe pia katika kuhakikisha kuwa nyaya za umeme zinasukwa na wale tu wenye utaalam uliothibitishwa na Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* na matumizi ya vyombo vya umeme yanazingatia nguvu na uwezo wa vitoleo vya umeme vilivyoko.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako limepitisha Muswada wa Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Serikali kwa Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu wa mwaka 2004. Katika mazingira tuliyonayo hivi sasa tunahitaji kuwa na utaratibu endelevu ambao utaliwezesha Taifa kugharamia Elimu ya Juu. Sote tunatambua umuhimu wakuwapata wataalam wa fani mbalimbali na ambao watatoa mchango wao katika kuleta mabadiliko ya maisha ya Watanzania. Hivi sasa Taifa letu limewekeza sana katika elimu, kwa kuanzia elimu ya msingi, sekondari na hatimaye elimu ya juu. Matunda ya juhudi hizi yanaanza kuonekana katika ngazi ya sekondari ambapo watoto wengi wanaofaulu hubaki bila kupata nafasi ya kujiunga na elimu hiyo. Hali hiyo ipo pia kwa elimu ya juu na itazidi kuwa mbaya jinsi Mpango wa Uboreshaji Elimu utakavyopanda hadi ngazi ya sekondari hasa ngazi ya *Advanced Level.* Kwa hali hiyo, lazima tujiandae kuwaingiza vijana wengi katika elimu ya juu kuliko ilivyo hivi sasa.

Katika mfumo wa elimu tulionao sasa ambapo sekta binafsi imepewa fursa za kuwekeza katika elimu ikiwa ni pamoja na elimu ya juu, ni vema tukaweka utaratibu ambao wanafunzi wengi kadri uwezo utakavyoruhusu na wanapotimiza masharti yaliyopo, wakawezeshwa kupata elimu hiyo ya juu. Utaratibu wa mikopo ndio utaratibu endelevu na utakaowawezesha vijana wengi wa Kitanzania kujiunga na elimu ya juu. Utaratibu huo siyo mgeni na unatumika katika nchi nyingi na hata hapa kwetu. Tukumbuke watoto wanaojiunga na Vyuo Vikuu binafsi ni watoto wa Watanzania ambao hawana tofauti na wale watoto ambao wanabahatika kujiunga na vyuo vya Serikali. Ili watoto wetu wengi zaidi wapate fursa ya elimu ya juu, Muswada huo nilioutaja, una lengo la kuanzisha Bodi ambayo itakuwa inatoa mikopo kwa vijana ambao wanajiunga na elimu ya juu lakini wazazi wao hawana uwezo. Bodi hii kwa sheria, itahakikisha kuwa wale wanaopatiwa mikopo hiyo wanawajibika kurudisha mikopo yao baada ya kumaliza masomo yao wakiwa wamepata ajira au wanajitegemea. Fedha zinazorudishwa pamoja na fedha zinazotengwa na Serikali zitajenga mfuko mkubwa zaidi wenye nguvu utakaokuwa na uwezo wa kuwakopesha vijana wengi zaidi.

Hivyo, sheria hii ina lengo la kuwawezesha vijana wengi zaidi ambao wazazi wao hawana uwezo kujiunga na elimu ya juu kwa kutumia mikopo na siyo kuzuia au kuwakwaza watoto wa wazazi wasio na uwezo kama ambavyo imekuwa ikielezwa na baadhi ya watu.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu limepitisha vile vile Muswada wa Sheria ya Bidhaa za Maziwa wa mwaka 2004. Nchi yetu ni moja ya nchi chache katika Bara la Afrika yenye mifugo mingi. Tumeelezwa kwenye Mkutano huu kuwa idadi ya ng’ombe wa asili nchini imefikia takriban ng’ombe milioni 17 wanaofugwa katika mfumo huria.

Pamoja na wingi huu, bado wafugaji wetu hawajanufaika kikamilifu na raslimali hii. Muswada wa sheria uliopitishwa na Bunge lako Tukufu unatupa fursa ya kujenga mazingira yatakayowezesha uzalishaji wa maziwa kukua kwa kuweka utaratibu kwa kuboresha mazingira ya wafugaji. Bado tunalo tatizo la wafugaji wanaohamahama kutafuta malisho na maji kwa ajili ya mifugo yao.

Hata hivyo, viongozi hususan sisi wa kuchaguliwa tunao wajibu wa kuwaelimisha wafugaji katika Majimbo yetu kuwa mazingira yanabadilika sana na kwamba kadri Watanzania watakavyohamasika zaidi katika masuala ya umiliki wa ardhi ndiyo wale wanaohamahama watakapojikuta hawana ardhi wanayoweza kuimiliki kwa ajili ya mifugo yao.

Kwa msingi huo, ni vyema katika upangaji wa matumizi ya ardhi, ardhi inayofaa kwa mifugo itengwe na wafugaji waelimishwe kuhusu umilikaji wa ardhi kama hiyo ili waweze kushiriki katika kuweka miundombinu mbalimbali. Wafugaji wetu wana mifugo mingi hivyo siyo watu maskini bali wanahitaji kuelimishwa na kuhamasishwa ili waweze kutumia raslimali yao kwa maendeleo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu tuchukue hatua za kurekebisha uchumi, yamekuwepo mabadiliko makubwa katika sekta mbalimbali. Uwekezaji umeongezeka katika nyanja karibu zote na ajira kwenye sekta rasmi nayo imeongezeka. Ingawa bado Serikali ndiyo mwajiri mkuu, sekta binafsi inakua na hivyo idadi ya wafanyakazi katika sekta hiyo inaongezeka kwa haraka. Vile vile yapo mabadiliko yanayotokea Kimataifa yanayoletwa na utandawazi na mabadiliko makubwa ya kiteknolojia. *(Makofi)*

Aidha, maamuzi yetu ya kuimarisha uhusiano wa Kikanda na katika Jumuiya ya Afrika Mashariki yanatoa changamoto kwetu kujaribu kuangalia mazingira yetu kila mara ili tuweze kufaidika na fursa mbalimbali zinazotokana na mabadiliko yote hayo. Eneo moja ambalo hatuna budi kuliangalia ni lile la mazingira na mahusiano katika kazi na vile vile Taasisi zetu za kazi. Hatua zote tunazozichukua za kurekebisha uchumi, lengo mojawapo ni kukuza ajira. Hata hivyo, Wawekezaji wengi wa ndani na hata kutoka nje, walianza kuona kuwa sheria zetu za kazi ni kikwazo katika kuongeza tija maeneo ya kazi. Mfumo wa uchumi wetu umebadilika kutoka uchumi hodhi uliokuwa unaongozwa na Serikali na vyombo vyake na kuwa uchumi huria unaoongozwa na nguvu za soko na sekta binafsi. *(Makofi)*

Kigezo kikubwa cha ufanisi wa uchumi huu unaoongozwa na soko na sekta binafsi, ni ongezeko la tija kwa gharama ndogo. Kwa msingi huo, Muswada wa Sheria ya Ajira na Mahusiano katika kazi wa mwaka 2003 na ule wa Sheria ya Taasisi za Kazi wa mwaka 2003, ina lengo la kujenga mazingira muafaka kwa pande zote yaani upande wa waajiri na upande wa wafanyakazi. *(Makofi)*

Kama alivyoeleza Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, ni lazima sasa Watanzania tubadilike na tutambue kwamba tija katika sehemu za kazi ndiyo tu itakayowezesha uchumi wetu kuendelea kukua. Tupige vita hatua zozote ambazo zitaleta migogoro katika maeneo ya kazi. *(Makofi)*

Wapo wanaodai kuwa Muswada wa Sheria ya Ajira na Mahusiano katika Kazi unawapendelea zaidi waajiri na kuwapa nguvu za kuwanyanyasa wafanyakazi. Napenda kuwahakikishia wananchi kwa ujumla na hususan wafanyakazi wote kuwa Muswada uliopitishwa na Bunge umezingatia maslahi ya pande zote na kwamba vyombo vya wafanyakazi vya kutetea na kulinda maslahi yao bado vitaendelea kuwepo. Tukumbuke tu kuwa uwazi wa masoko pia ni kwa soko la ajira na tukumbuke pia kuwa bidhaa zetu hazina soko la peke yake bali zitashindana na bidhaa za wengine kwa ubora na unafuu wa bei katika masoko ya pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nguzo muhimu ya bajeti ya Serikali ni mapato yatokanayo na kodi mbalimbali. Katika kipindi cha karibu miaka tisa sasa tumefanya kazi nzuri ya kukusanya mapato kwa kutumia sheria zilizopo. Matokeo ya juhudi hizi ni kuwa mapato yetu ya ndani yameongezeka kutoka wastani wa shilingi bilioni ishirini na tano kwa mwezi mwaka 1995/96 hadi wastani wa shilingi bilioni mia moja na nane kwa mwezi mwaka 2003/2004. *(Makofi)*

Hata hivyo, kiwango hiki tulichofikia ni asilimia 12.8 tu ya pato la Taifa kwa mwaka. Wataalam wanatueleza kuwa ili kuwa na uwiano mzuri wa makusanyo ya mapato ya ndani yanayoweza kukidhi mahitaji yetu muhimu, tunahitaji kufikia kiwango cha zaidi ya asilimia ishirini ya pato la Taifa. Kutofikiwa kwa kiwango hicho, ndicho kinachosababisha bajeti yetu bado iwe tegemezi kwa asilimia 45 na zaidi. Muswada wa Sheria ya Kodi ya Mapato wa Mwaka 2004 una lengo la kututoa katika hali hiyo ya kuwa tegemezi kwa kupanua wigo wa mapato kwa kuanzisha vyanzo vipya ili kila anayestahili kulipa kodi alipe kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato nchini imefanya kazi kubwa na nzuri na sote tunajivunia mafanikio yao. Lakini pamoja na mafanikio hayo, bado tunayo nafasi kubwa ya kuongeza mapato yetu. Sheria hii mpya ya Kodi ya Mapato ina lengo la kuingiza utaratibu wa walipa kodi wetu kujikadiria kodi na hivyo kuwajibika kwa kodi wanayolipa. Utaratibu huu ni mpya na kwa awali tunaanza na makampuni na watu binafsi watajiunga nao baada ya elimu kutolewa kwa umma. Lengo kuu ni kujiongezea mapato na Watanzania kuwajibika zaidi katika ulipaji kodi. Juhudi hizi ni muhimu ili tusiendelee kuwa tegemezi daima kwani sote tunatambua athari za kuendelea kuwa tegemezi. Utegemezi unatupunguzia uhuru wetu wa kufanya maamuzi ambayo wakati mwingine ni muhimu kwa maslahi ya Taifa letu. Ni mategemeo yangu kuwa utekelezaji wa sheria hiyo mpya utatuwezesha kufikia malengo tunayokusudia ya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu limepokea vile vile taarifa ya Kamati mbili za Kudumu za Bunge. Katika taarifa hizo, tumeelezwa kuhusu utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kisekta zenye malengo ya kuboresha maisha ya wananchi wetu na matatizo yanayokwamisha au kuchelewesha kufikiwa kwa malengo hayo. Serikali imepokea taarifa hizo na itazingatia ushauri wa kila Kamati kadri itakavyowezekana na kulingana na uwezo wetu kibajeti pale fedha zinapohitajika ili tuweze sote kwa pamoja kuwasaidia wananchi kupambana kikamilifu na umaskini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha karibu miezi miwili yaani mwezi Machi na Aprili, 2004 mvua zimenyesha karibu maeneo yote nchini na kuanza kuleta matumaini makubwa kwa wakulima na wananchi wetu kwa jumla. Taarifa zinaonyesha kuwa karibu maeneo mengi nchini, mazao ni mazuri na kwamba upo uwezekano mkubwa wa kupata mavuno ya kuridhisha.

Hata hivyo, yapo baadhi ya maeneo machache ambayo mvua zilichelewa na hivyo mazao ya wakulima kunyauka. Sote tu mashahidi wa jinsi ukame wa kipindi kirefu mwaka jana na mwanzoni mwa mwaka huu ulivyosababisha upungufu mkubwa wa chakula.

Kwa vile sasa wakulima wameanza kupata matumaini ya kuvuna mazao, ni vyema sisi viongozi na wataalam tuanze kuwahimiza wananchi wetu wajitayarishe kwa kujiwekea akiba ya chakula. Tuwahimize na kuwahamasisha wananchi watumie taratibu zote wanazozifahamu za hifadhi ya nafaka za chakula. Watendaji wote wa Vijiji hadi watendaji wakuu wa Halmashauri zetu chini ya uongozi wa Wakuu wa Wilaya wahakikishe kuwa kwa yale maeneo ambayo wakulima wana mategemeo ya kuvuna vizuri kila familia inakuwa na ghala ya akiba ya chakula.

Kazi ya kujiwekea akiba ya chakula ni sehemu ya utamaduni wa wakulima wengi nchini. Kwa msingi huo, hili siyo suala jipya ni suala linalohitaji kusimamiwa kwa karibu na watendaji na viongozi. Viongozi wa Wilaya wote nchini walisimamie suala hili kikamilifu katika kipindi hiki cha mavuno. Ni vema wananchi wakaendelea kukumbushwa kuwa jukumu la kwanza la kulisha familia ni la kila mkuu wa kaya mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo tulipata matatizo sana katika msimu uliopita ni lile la kupungua sana kwa maji katika Bwawa la Mtera hivyo kuathiri uzalishaji wa umeme. Pamoja na kuwa hali ya ukame imechangia kwa sehemu kubwa kupungua kwa maji katika bwana hilo, hali ya uharibifu wa mazingira katika maeneo ya vyanzo vya mito, vijito na chemichemi zinazoingiza maji kwenye bwawa hilo nayo imechangia sana upungufu huo wa maji. Hivi sasa bado mitambo ya Mtera imefungwa na licha ya mvua za kuridhisha zilizonyesha katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini bado maji yaliyoingia kwenye bwawa hilo hayajaweza kujaza na kufikisha kiwango cha bwawa hilo kuweza kutumika kwa uzalishaji wa umeme.

Pamoja na ukweli kuwa katika kipindi kifupi kijacho, uvunaji wa gesi ya Songosongo utaanza na hivyo kuwezesha uzalishaji wa umeme unaotokana na gesi asilia, bado tutaendelea kutegemea umeme unaotokana na nguvu za maji kwa vile miundombinu hiyo ipo, gharama yake ni nafuu na hivyo vyanzo vingine uwezo wao bado ni mdogo. Kwa msingi huo, ni vema kama Taifa tuanze sasa kuchukua hatua za dhati hata kama zitakuwa chungu ili kulinda vyanzo vya maji na bwawa lenyewe la Mtera. *(Makofi)*

Kwa kuanzia ni wajibu wa viongozi na watendaji wa Mikoa yote ambayo ina vyanzo vya maji ya bwawa la Mtera wakutane na kuweka mipango na mikakati ya

kuhifadhi maeneo yote yanayohusika. Hatuwezi tena kulipuuzia suala hili kwani athari zake kwa uchumi na maendeleo yetu yapo dhahiri na tumeyaona. Katika kutekeleza suala hili, ni vema wananchi washirikishwe kikamilifu kwa kuhamasishwa na kuelimishwa ili watambue wajibu wao lakini vile vile washiriki kikamilifu katika hifadhi ya maeneo yote yanayohusika. Eneo la vyanzo vya mito vya Bwawa la Mtera ni hifadhi ya Taifa ya msitu lakini bado watu wanachungia mifugo katika eneo hilo na kulima katika maeneo hayo ya msitu. Hifadhi hiyo sasa isimamiwe na walioko milimani katika maeneo hayo watolewe mara moja ili kunusuru uhai wa bwawa la Mtera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tupo katika robo ya mwisho ya mwaka wa fedha 2003/2004, katika kipindi cha takribani miezi tisa, Serikali imekuwa ikitekeleza bajeti na mipango iliyoidhinishwa na Bunge lako katika mwaka huu wa fedha. Tumekumbana na matatizo makubwa ya ukame na upungufu wa umeme na tumeweza kukabiliana navyo kwa kiwango cha kuridhisha. Tunapoelekea mwishoni mwa mwaka wa fedha, tunalo jukumu sisi kama wawakilishi wa wananchi kushirikiana na watendaji katika ngazi za Halmashauri zetu ili pale ambapo matatizo ya utekelezaji siyo makubwa, tuweze kutimiza malengo tuliyojiwekea katika mwaka huu wa fedha. Wakati huu vilevile ndicho kipindi ambacho Serikali ipo katika hatua muhimu za matayarisho ya bajeti na mpango wa mwaka 2004/2005. Wito wangu kwa sekta binafsi ni kuwa washirikiane na Serikali kama ilivyokuwa miaka ya nyuma ili tuweze kutengeneza bajeti ya Serikali itakayotuongezea nguvu kubwa ya kuongeza uzalishaji na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Serikali na mpango wa mwaka una madhumuni makuu ya kujenga mazingira yatakayowezesha Watanzania kupambana na umaskini. Katika utekelezaji wake, tunahitaji usimamizi na uongozi imara hususan kutoka kwa viongozi na watendaji walio karibu zaidi na wananchi. Ni wajibu wa viongozi na watendaji hao kuonyesha ubunifu utakaowezesha kutumia raslimali chache zinazotolewa na Serikali kama chachu ya kuleta mabadiliko katika vijiji na mitaa nchini. Ni wajibu wao vilevile kutumia fursa zinazojitokeza kujifunza kutoka kwa wenzao waliopata mafanikio zaidi.

Kwa mfano, tunayo mikoa ambayo imefanikiwa sana kwa kilimo cha mazao ya chakula. Siyo vibaya kwa wale ambao wapo nyuma katika eneo kama hili wakijifunza kutoka kwa wenzao ambao wamefanikiwa. Ninachotaka kusisitiza hapo ni umuhimu wa viongozi na watendaji wa Serikali kubadilishana uzoefu na kujifunza mbinu mbalimbali za kuwawezesha wananchi kutekeleza na kufanikisha malengo waliyojiwekea katika sekta mbalimbali za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Spika, kuanzia tarehe 19 Aprili, 2003 tumeanza maadhimisho ya Juma la Elimu kwa Wote. Kama alivyoeleza Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Joseph Mungai, maadhimisho haya ni fursa kwetu Watanzania kuthamini elimu na kutoa msukumo mkubwa zaidi kama Taifa na familia moja moja kuhakikisha kuwa tunawawezesha watoto wote wa Kitanzania kupata elimu bila ubaguzi wa kijinsia au ubaguzi mwingine wa aina yoyote. *(Makofi)*

Katika ziara zangu Mikoani, nimekuwa nikisisitiza suala la elimu hususan ya watoto wa kike kwa sababu bado wapo baadhi ya Watanzania ambao hawajali elimu kwa watoto wa kike. Napenda kutumia fursa hii kuwataka viongozi tangu ngazi ya vijiji hadi Wilayani kuendelea kusimamia suala la kupiga vita utoro wa watoto mashuleni na kuchukua hatua za kisheria kwa wale wote watakaowakatiza watoto masomo kwa sababu yoyote ile. *(Makofi)*

Sote tumesikia kutoka kwa Waziri wa Elimu na Utamaduni jinsi Taifa letu lilivyopiga hatua kubwa katika utekelezaji wa maazimio ya Dakar-Senegal ya elimu kwa wote wa mwaka 2000. Ni wajibu wetu sasa kusimamia mafanikio hayo ili yawe endelevu kwa kuondoa kasoro au upungufu wowote uliopo hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 17 Aprili, 2004 baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kukutana na wawakilishi wa Makampuni tisa ya Kitanzania yaliyopata tuzo kwa ubora wa bidhaa na huduma; matumizi ya teknolojia na uongozi. Ni faraja kubwa kwetu tunapoona jinsi Watanzania tunavyoanza kubadilika na kutumia changamoto mbalimbali zinazojitokeza kuboresha huduma na bidhaa. Tumeanza sasa kutambua, japo bado siyo kwa kasi tunayoitaka, kuwa katika ulimwengu huu wa ushindani ubora wa huduma na bidhaa na ongezeko la tija ndizo nguvu kubwa zitakazotuwezesha kuingia katika soko la Mataifa. Kama ninavyosema kila mara haitusaidii kuulalamikia au hata kuulaani utandawazi kwani upo na utaendelea kuwepo. Bali ni sisi wenyewe kuutumia utandawazi huo kikamilifu kwa faida na maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, makampuni hayo na mengine ya Kitanzania ambayo yameonyesha uwezo huu yawe kichocheo kwa wengine kwani kuboreka kwa huduma na bidhaa kutatuwezesha kuingia katika biashara ya Kimataifa bila matatizo. Napenda kuwahakikishia wafanyabiashara na wawekezaji wote kuwa Serikali itaendelea kusaidiana nao katika kuendelea kuboresha mazingira yetu ya biashara na uwekezaji ili kuwawezesha kutimiza malengo yao, kuongeza ajira na kuleta utajiri katika nchi yetu. Napenda kutoa pongezi sana kwa zile kampuni tisa kwa kufanya vizuri na kupewa tuzo za Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jumatatu ijayo yaani tarehe 26/4/2004, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar unatimiza miaka arobaini tangu uasisiwe. Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza kwa dhati waasisi wa Taifa letu, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Abeid Aman Karume, kwa upeo wao wa kuona mbali na kutuunganisha Watanganyika na Wazanzibar na kuwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wao walitambua umuhimu wa Muungano na walikubali kwa dhati kuweka maslahi ya wananchi wa pande zote mbili za Bara na Visiwani mbele kuliko maslahi yao binafsi. Leo, miaka arobaini baada ya kuasisiwa kwa Muungano wetu, Watanzania tuna fahari sana na Muungano huo na tunaona umuhimu wake. Katika kipindi hiki vilevile Watanzania wa pande zote mbili tumekubali kwa dhati kujenga misingi ya Utaifa ambayo inatuweka pamoja. Hili ni jambo la kihistoria ambalo hatuwezi kuliondoa. Wapo watu wengi sana wenye asili ya Bara waliohamia

Visiwani kwa sababu za kibiashara au nyingine miaka mingi iliyopita na vivyo hivyo kwa wale wa Visiwani. Kwa sababu hiyo siyo rahisi kwa Muungano wetu kuvunjika kwani msingi wake ni zaidi ya taasisi au vyombo tulivyovianzisha baada ya mwaka 1964. Huu ni Muungano wa watu wenyewe na kwamba waasisi wetu walihalalisha kisheria na Kikatiba undugu uliokuwepo baina yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miaka arobaini siyo muda mfupi. Katika kipindi hicho Muungano wetu umepita katika hatua mbalimbali, tumepata mafanikio mengi sana, lakini pia tumekumbana na matatizo kadhaa. Katika wakati wote huo tumetatua matatizo yetu kama ndugu na kwa maelewano makubwa. Hata hivyo, kama nilivyowahi kulieleza Bunge lako Tukufu, matatizo haya ni ya kitaasisi zaidi na kwamba wananchi wenyewe hawana matatizo. Tunapoadhimisha siku hiyo muhimu kwa Taifa letu, Watanzania hatuna budi kupiga vita kwa nguvu zetu zote kauli na hata vitendo kama vipo vyenye nia ya kudhoofisha au hata kuvunja Muungano wetu. Kwa niaba yenu Waheshimiwa Wabunge ninapenda niwapongeze kwa dhati Marais wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa na Mheshimiwa Amani Abeid Karume na Watanzania wote kwa kuadhimisha miaka 40 ya Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu ni Mkutano wa kumi na tano wa Bunge lako Tukufu, hivyo bado Mikutano mitano tu au bado miezi kumi na tano tu Bunge hili limaze muda wa uhai wake. Hii maana yake ni kuwa maandalizi ya Uchaguzi Mkuu nayo yameanza na joto la siasa limeanza kupanda katika Majimbo yetu, katika Vyama vyetu, baina ya Vyama vyetu na hata kwa wananchi wenyewe. Mwaka huu mwezi Novemba, (2004) tutakuwa na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa ngazi za Vitongoji, Vijiji na Mitaa. Wadau wote hivi sasa wamekwishakutana na wametoa mapendekezo yao kuhusu kanuni za Uchaguzi huo. Wizara husika, TAMISEMI hivi sasa inaandaa kanuni hizo na zitasambazwa kwa muda muafaka kunakohusika. Hata hivyo, ni wajibu wetu ndani ya Serikali, Vyama vya Siasa na Asasi zisizo za Kiserikali kutoa elimu kwa wananchi kuhusu uchaguzi huo ili tuendelee kuimarisha demokrasia yetu katika ngazi hizo. Mara ya mwisho, uchaguzi kama huo ulifanyika mwaka 1999. Matarajio yetu ni kuwa Vyama vyote vyenye usajili wa kudumu vitashiriki kikamilifu katika uchaguzi huo wa mwaka huu kama vilivyofanywa kwa uchaguzi wa 1999. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mara baada ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa, uchaguzi unaofuatia ni Uchaguzi Mkuu kwa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Zanzibar, Wabunge, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani. Tume zetu za Uchaguzi zinaendelea na matayarisho muhimu ikiwa ni pamoja na maandalizi ya daftari za kudumu za wapiga kura. Daftari hizi zina umuhimu sana ili kuziba mianya inayoweza kutumika kwa urahisi kuingiza udanganyifu katika upigaji kura. Kuna Vyama vya Siasa vilivyosikika vikiwaambia wananchi kuwa wasikubali kujiandikisha katika daftari hili la wapiga kura. Hatujaelewa tatizo ni nini kwa sababu Vyama hivyo hivyo ndivyo vilivyotishia kususia Uchaguzi kama hapatakuwa na daftari la kudumu la wapiga kura. Ninawahimiza sana Watanzania wote wenye umri wa kupiga kura wajiandikishe wakati muafaka utakapofika ili wasije wakapoteza haki yao ya kupiga kura kuchagua viongozi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, joto la siasa limeanza kupanda katika maeneo mengi na hata katika Vyama vyetu. Tayari watu wameanza kushutumiana na lugha za vitisho na hata vitendo vya vitisho vimeanza kujitokeza kutoka baadhi ya Vyama vya Siasa. Pamoja na kuwa ni kawaida kwa joto kupanda nyakati kama hizi, ni vyema viongozi wa kisiasa wakajua kuwa wana jukumu kubwa la kutoa uongozi kwa wanachama wao na wananchi kwa ujumla. Hazina kubwa ya Watanzania ni amani, utulivu na mshikamano wao. Wanasiasa ni lazima tujue kuwa tuna jukumu kubwa la kulinda amani na utulivu huo. Tusijenge mazingira yanayoweza kuhatarisha amani na mshikamano wa Watanzania kwa maslahi yetu ya kisiasa.

Wapo wanaotangaza chuki hata kutaka kuwahamisha watu kutoka eneo moja la Jamhuri kwenda eneo lingine, wapo wanaotengeneza makundi kwa misingi ya dini, wapo wanaoanza kupanga wagombea kwa misingi ya ukabila na ukanda na kadhalika. Haya yote ni mambo ya hatari kwa umoja wetu na mshikamano wetu. Ni vyema wenye tabia hiyo wakaacha mara moja. Tanzania ni nchi yetu sote na hakuna mtu anayekatazwa kwenda kuishi popote nchini na kushiriki shughuli za siasa ama kwa kugombea au kuchagua. Aidha, hakuna kiongozi yeyote atakayeshinda uchaguzi kwa tiketi ya udini, ukabila au ukanda. Tuepuke sana mambo hayo yanayoweza kuwagawa Watanzania. Ninapenda kuwahakikishia Watanzania wote wa Bara na Visiwani kuwa Serikali zao ziko macho, zitawalinda na zitapambana na vitendo vyote viovu vinavyotaka kuharibu amani, utulivu na mshikamano wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda nikushukuru kwa dhati wewe binafsi kwa kutuongoza hadi tumefanikiwa kukamilisha shughuli zote zilizopangwa kwa ajili ya Mkutano huu. Aidha, ninawashukuru Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti, Naibu Spika na Mbunge wa Tunduru na Wenyeviti, Mheshimiwa Eliachim Simpasa na Mheshimiwa Anne Makinda, kwa msaada waliokupa katika kuongoza Mkutano huu. Napenda vilevile kwa niaba ya Bunge hili kuwashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge, chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Mheshimiwa Kipenka Mussa, kwa huduma mbalimbali walizotoa kwetu na ambazo zimetuwezesha kutekeleza majukumu yetu. Nawashukuru pia wafanyakazi wote wa Serikali na Mashirika ya Umma kwa juhudi zao za kuhakikisha kuwa majukumu ya Serikali yametekelezwa kwa ufanisi mkubwa kulingana na kanuni na taratibu za Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, napenda vile vile kuvishukuru vyombo vyote vya habari kwa kuendelea kutekeleza wajibu wao kikamilifu. Wananchi wengi wanapenda kufuatilia masuala yanayoshughulikiwa na Wawakilishi wao katika Mikutano ya Bunge. Vyombo vya habari vimefanikiwa sana kuamsha msisimko wa wananchi kupenda kufuatilia shughuli hizo za Bunge. Endeleeni na kazi hii nzuri na kila mara mpende kuiboresha zaidi ili wananchi waendelee kufuatilia shughuli za Bunge na kwa kufanya hivyo tutaweza kujenga misingi imara ya chombo hiki cha uwakilishi wa wananchi. Baada ya maelezo haya, sasa naomba kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu liahirishwe sasa hadi tarehe 8 Juni, 2004, siku ya Jumanne Saa Tatu Asubuhi, litakapokutana hapa Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Saa 11.38 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 8 Juni, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*